13.1: MAELEZO YA JUMLA JUU YA SIKU 10 ZA MAFUNZO KWA WAKUFUNZI YA VYOTE UNAVYOPASWA KUJUA KUHUSU VIAZI
VITAMU..... 362

13.2:MAELEZO YA JUMLA JUU YA SIKU 5 ZA KOZI YA MAFUNZO KWA WAKUFUNZI YA VYOTE UNAVYOPASWA KUJUA KUHUSU
VIAZI VITAMU 381

13.3: MAWASILISHO YAAMBATANAYO NA KOZI YA MAFUNZO KWA WAKUFUNZI YA 'VYOTE UNAVYOPASWA KUJUA KUHUSU
VIAZI VITAMU 391

13.4: KADI ZA KUSAIDIA KUMBUKUMBU ZA KOZI YA MAFUNZO KWA WAKUFUNZI YA VYOTE UNAVYOPASWA KUJUA KUHUSU
VIAZI VITAMU 392



Mada ya 13: Namna ya Kutumia Kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi ya Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu

13.1: Maelezo ya jumla juu ya siku 10 za mafunzo kwa wakufunzi ya Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu

Mafunzo haya ya kujifunza kwa vitendo yamesanifiwa ili kutoa fursa kwa washiriki kujifunza kwa njia ya kugundua kati ya siku kumi za kozi ya *Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu: Kitabu cha mafunzo kwa wakufunzi cha mradi wa kuwasaidia wadau wa mabadiliko*. Tunatumaini kuwa mkiendelea kujifunza kuhusu viazi vitamu, kama wakufunzi mtajikuta mnawafunza wengine kwa kupitia mkakati wa mafunzo kwa vitendo.

Programu nzima ya siku 10 zilizoshauriwa ya mafunzo kwa wakufunzi imeelezewa hapa (Jedwali la 13.1), na siku 5 za mafunzo kwa wakufunzi zilizoshauriwa zimefafanuliwa katika Kipengele cha 13.2. Programu hii inalenga kuwasaidia wawezeshaji weledi katika mipango yao. Lakini haikusudiwi kuelezea tu. Tafadhali tumia ubunifu wako kulingana na mahitaji ya washiriki.

Matarajio ya jumla ya somo la *Vyote Unavyopaswa Kujua Kuhusu Viazi Vitamu*: Kwa kutumia kanuni na mikakati iliyotolewa wakati wa siku 10 za kozi utawafanya washiriki waweze:

- kuelewa mambo muhimu ya uzalishaji wa viazi vitamu, matumizi na uuzaji/soko katika Afrika Kusini chini ya Jangwa la Sahara;
- kuonyesha ujuzi muhimu kama vile uchaguzi na usimamizi wa magonjwa, na maandalizi ya visaidizi vya mwelekeo wa ukuaji viazi vitamu;
- kuelewa/kufahamu kuhusu umuhimu wa vitamini A katika mlo wa binadamu na njia ambazo viazi vitamu lishe na vyakula vingine vinaweza kutumika kuepuka upungufu wa vitamini A;
- kuelewa ni vipi shughuli za kijinsia zinavyoathiri uzalishaji wa viazi vitamu;
- kujiamini katika kutoa mafunzo juu ya viazi vitamu hasa kwenye eneo la utafiti/uzalishaji, maafisa kilimo/ugani na wafanyakazi wa mashirika yasiyo ya kiserikali kwa kujifunza kwa vitendo kupitia mfumo wa ubunifu na kujifunza kwa ugunduzi.

Washiriki walengwa: Maafisa ugani katika ngazi ya wilaya, wafanyakazi wa taasisi zisizo za kiserikali (NGOs), watafiti wa kilimo wa kitaifa, wagani wa lishe/afya. Washiriki hawa wana wajibu wa kuwafunza watu binafsi na maafisa ugani wa umma ngazi ya chini ambao nao mwishoni watawafunza wakulima.

Programu iliyopo hapa chini inaelezea mada, matokeo ya somo lililokusudiwa na shughuli zilizoshauriwa kwa kila siku kati ya siku 10 za Mafunzo kwa Wakufunzi. Maelezo ya kina ya hatua kwa hatua kwa kila zoezi la mafunzo kwa vitendo yanapatikana kwenye mada za mwanzoni. Kwa mfano Zoezi la 1.3.1 litapatikana katika Kipengele cha 1.3 cha kitabu hiki.

Maelekezo ya kina ya hatua kwa hatua kwa kila zoezi la mafunzo kwa vitendo yanaainisha matarajio ya somo yaliyokusudiwa, muda uliotarajiwa kwa zoezi (na kila hatua yake), maandalizi ya awali yanayohitajika, zana zinazohitajika, na mapendekezo ya hatua kwa hatua wakati mwezeshaji anapokuwa anasaidia ufanyaji zoezi.

Maandalizi ya awali yanayohitajika yanaelezewa kwenye mstari wima wa sehemu ya mwisho ya ledwali la programu nzima. Yanagusia umuhimu wa kuandaa ziara za mashambani na kwenye masoko mapema, hususan kama shamba linatakiwa lipandwe mazao kwa ajili ya mafunzo. Mazoezi ya viazi vitamu kwa vitendo ndiyo yanayochukua nafasi kubwa ya uwanja wa mafunzo kwa kozi zote za mafunzo kwa wakufunzi ya siku 10 na ile ya siku 5. Mashamba ya mafunzo haya ya viazi vitamu yanapaswa kuwa maeneo jirani; yaliyopandwa aina mbalimbali za viazi vitamu na yawe na mimea ya viazi vitamu itakayokuwa na miche iliyokomaa na viazi vyenyewe wakati wa

mafunzo. Inapendekezwa mashamba yawe na viazi vitamu vilivyokwisha athiriwa na virusi na wadudu waharibifu; mashamba yawe yale yanayomilikiwa na wakulima walio tayari kuruhusu washiriki kukata vipandikizi vichache wanapokuwa wanajifunza namna ya kuchagua vipando salama, na kuchimbua mimea michache ili kutafiti namna viazi vinavyokua na kujifunza kuhusu uvunaji, na ambao kwa hakika watarudishiwa gharama za mimea na viazi vyao.

Ni vyema zaidi kuwe na mashamba ya wakulima jirani, na kijaruba cha karibu ambacho washiriki watafanya majaribio ya kuandaa vitalu vya uzalishaji haraka, na uhifadhi wa viazi vitamu vibichi. Muda unaoshauriwa kwa ajili ya shughuli za maandalizi unaonyeshwa kwenye Jedwali la 13.2.

Jedwali la 13.1: Programu/Mpango kwa ajili ya siku 10 za Kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi itakayokujuza mambo upaswayo kujua kuhusu viazi vitamu

| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
|------|---|---|--|---|
| 1 | <p><i>Utangulizi</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Matarajio ya washiriki, makubaliano juu ya matokeo ya kujifunza. - Mtazamo wa jumla wa umuhimu na matumizi ya viazi vitamu. - Namna jinsia na anuwai zinavyohusiana na shughuli za viazi vitamu. | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuelewa mpango/ programu ya kozi na jinsi ilivyolenga kuwaandaa wakufunzi kwa ajili ya kuwafunza wengine juu ya viazi vitamu. - Kufahamu kuhusu mienendo na changamoto za uzalishaji wa viazi vitamu na matumizi yake. - Kuwa na uwezo wa kuelewa ni kwa nini masuala ya jinsia na anuwai ni muhimu kwenye mnyororo wote wa viazi vitamu. - Kuandaa milo miwili ya viazi vitamu. | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Utangulizi:</i> Kazi ya vikundi (dakika 30) - <i>Matarajio:</i> Kuyaweka matarajio ya washiriki katika makundi na kushirikiana pamoja (utambulisho wa kila mmoja) na kuweka hatua moja iliyosawa kwa mujibu wa matarajio ya wakufunzi na baadaye kuweka sawa matokeo yaliyopo ya kujifunza na kisha kuyajadili tena ikiwezekana. (dakika 45) - <i>Zoezi la kuingilia:</i> Zoezi la uelewa kuhusu ufahamu wa viazi vitamu mwanzoni mwa mafunzo/kozi inapoanza (Kiambatanisho cha 1.2). - <i>Programu:</i> Mtazamo wa jumla wa mpango wa programu ya kozi ya mafunzo kwa wakufunzi (dakika 10). - <i>Historia na elimu ya viazi vitamu:</i> Kazi ya vikundi vidogo vikishughulika juu ya ufahamu wa washiriki kuhusu historia ya viazi vitamu, umuhimu wake kitamaduni, uzalishaji na mienendo ya matumizi yake, na matatizo sugu yanayowakumba wakulima wa viazi vitamu (dakika 30 kwa kazi za vikundi, dakika 5 kwa ajili ya kuwasilisha mambo ya msingi kwa kila kundi). - <i>Kupika vyakula vya viazi vitamu lishe:</i> Makundi kupika vyakula vya viazi vitamu lishe (uji wa viazi vitamu au maandazi) tazama namba 9.4 kwa ajili ya kupata | <ul style="list-style-type: none"> - Chati mgeuzo, kalamu za wino mnene, gundi, stika/vibandikizi. - Nakala za jaribio la ufahamu wa viazi vitamu (Kiambatanisho cha 1.2). - Mtazamo wa jumla wa programu ya mafunzo. (Siku na Mada) - Viungo na vyombo vya kupikia na vifaa na mafuta ya kuwashia moto ili makundi yaandae uji wa viazi vitamu lishe na maandazi (kutumia mapishi yaliyoelezwa kwenye Zoezi la 9.4.1 na 9.4.2); <p><i>Uji wa viazi vitamu lishe:</i> Viungo kwa ajili ya watu 4 na zidisha kadri inavyohitajika unga wa viazi vitamu uliojaa kijiko kimoja cha chakula; unga wa mtama/uwele vijiko 4 vya chakula; unga wa mahindi au muhogo, unga wa soya kijiko 1 cha chakula; limau 1 dogo; vijiko 2 vikubwa vya sukari; vikombe 6 vya maji; vikombe; sufuria; jiko; panga; upawa wa mbao; vijiko vya chakula.</p> <p><i>Maandazi ya viazi vitamu lishe:</i> Viungo kwa watu 10 na zidisha kadri inavyohitajika: ½ kikombe cha viazi vitamu vilivyoondwa (vilivyoandaliwa kabla) au unga wa viazi vitamu (30%); vikombe 2 vya unga wa ngano (70%); sukari vijiko 2 vikubwa; vidonge vya chumvi; mafuta ya kupikia vikombe 2; hamira kijiko 1; maji ya kutosha ya</p> |

| | | | | |
|--|--|--|---|---|
| | | | <p>kwa kina viini vilivyopo na mchanganyiko wake. (Saa 1 na nusu)</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho</i>: Asili na umuhimu wa viazi vitamu (Mada ya 2), ikifuatiwa na mjadala wa makundi. (dakika 45) - <i>Wasilisho la 11</i>: Jinsia na anuwai na namna ilivyo na umuhimu kwenye shughuli za viazi vitamu (Mada ya 11) ikifuatiwa na mjadala ya vikundi. [dakika 45] | <p>vuguvugu; bakuli la kuchanganyia; chekeche; mti wa kusukumia; kikaangio; jiko; bakuli la kupakulia.</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 2</i>: Chanzo na umuhimu wa viazi vitamu. <i>Wasilisho la 11</i>: Jinsia na anuwai na umuhimu wake kwenye shughuli za viazi vitamu. |
|--|--|--|---|---|

| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/ Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
|------|---|--|---|--|
| 2 | Aina mbalimbali za viazi vitamu na sifa zake. | <p><i>Washiriki waweze</i>:</p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuelewa tofauti kuu zilizopo kati ya aina mbalimbali za viazi vitamu. - Kufahamu kuhusu sifa kuu za angalau aina 3 za viazi vitamu ambavyo vinaweza kufaa katika maeneo/ miko ya yao. - Kuwa na uwezo wa kuwasaidia wakulima kutambua sifa kuu wanazozitafuta katika aina fulani ya viazi vitamu. - Kuelewa/ kufahamu | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 3.5.1: Kubaini tofauti</i>. Shughuli ya shamba ili: - Kubaini sifa za aina mbalimbali za viazi vitamu katika eneo jirani la utafiti; kujadili na wakulima / mkulima juu ya kwa nini analima kila aina iliyopo ya viazi vitamu; na baada ya hapo mkulima atatumia viazi vya aina mbalimbali kufanya tathmini ya ladha ya viazi vitamu (angalia Kipengele cha 3.5.1). [saa 2 na dakika 45] - <i>Zoezi la 3.5.2: Kuchagua aina ya viazi vitamu</i>. Mjadala katika makundi juu ya vigezo vikuu vya kutofautisha aina mbalimbali za viazi vitamu na ni aina gani muhimu na kwa sababu zipi. Washiriki baadaye watatengeneza vipeperushi/vibandwikwa vya uboreshaji/zana za kufundishia kwa aina kuu za viazi vitamu | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 3.5.1</i>: Shamba jirani linalolimwa aina mbalimbali za viazi vitamu na washiriki kuwa na uwezo wa kuvuna kiasi fulani cha viazi, karatasi zenye ukubwa wa A4, karatasi nyeupe, penseli, vifutio, vijitabu vya kuchukua kumbukumbu, nakala za kutosha zinazofafanua juu ya viazi vitamu (Kiambatanisho cha 3.1), na namna ya kukisia kiwango cha vyanzo vya karotini kwa kutumia rangi ya njano ya aina ya viazi vitamu vibichi (Kiambatanisho cha 3.2), nakala za kutosha za fomu kwa ajili ya tathmini shirikishi ya ladha ya viazi vitamu (Fomu 5B na 5B2 Kiambatanisho cha 3.5b), majiko ya kupikia na mafuta ya kuwashia moto, vikaangio, maji, viberiti, visu. - <i>Zoezi la 3.5.2</i>: Chati mgeuzo (angalau ukurasa mmoja kwa kila mshiriki); penseli za rangi, |

| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/ Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
|------|------|---|---|--|
| | | <p>kwamba upendeleo wa aina fulani ya viazi vitamu utatofautiana baina ya watu.</p> <ul style="list-style-type: none"> - Kujulishwa juu ya kwa nini uangalifu wa viazi vitamu ni muhimu wakati wa mavuno. - Kufahamu namna ya kufanya zoezi la kuweka aina za viazi vitamu katika madaraja kulingana na ubora (kwa kutumia kadi zenye rangi nyekundu, njano na kijani). - Kuwa na uzoefu katika kufanya jaribio la ladha ya viazi vitamu (kwa kutumia kadi zenye rangi nyekundu, njano na kijani). | <p>vinavyozalishwa au aina zinazofaa katika maeneo yao (angalia Kipengele cha 3.5.2: Uchaguaji wa aina za viazi vitamu). [dakika 70]</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 3</i>: Kuangalia anuwai ya asili ya viazi vitamu; kuzitaja tabia za aina mbalimbali za viazi vitamu; njia za kufanya majaribio ya aina mbalimbali za viazi vitamu na mjadala shambani. [dakika 45] | <p>nyingi zikiwa za kijani, kahawia, chungwa na njano; katalogi ya CIP ya viazi vitamu vibichi rangi ya chungwa/njano.</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 3</i> juu ya anuwai ya viazi vitamu, sifa za aina mbalimbali na mbinu ya kujaribia aina mbalimbali za viazi vitamu. <p><i>Maandalizi ya awali: Kwa zoezi la 3.5.1</i>: Tambua eneo lililo jirani lililopandwa aina mbalimbali za viazi vitamu, na jaribu kukutana na wakulima na uangalie kama wanakubali mashamba yao yatembelewe na washiriki, wakulima kukubali kuhojiwa na washiriki, na baadhi yao wajaribu kupunguza idadi ya mimea/ miche ya viazi vitamu kwa kuchimba ili kuona tabia za viazi na kuondoa baadhi ya viazi kwa ajili ya kujaribu ladha, ikiwezekana mmea mmoja au mawili kwa kila aina ya viazi vitamu. Mkulima atahitaji afidiwe viazi viilivyovunwa na kuondolewa.</p> |

| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
|------|---------------|---|--|---|
| 3 | Lishe na OFSP | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuelewa mlo kamili ukoje na kwa nini ni muhimu. | <ul style="list-style-type: none"> - Kuchangiana mawazo: Mlo kamili ni nini? - <i>Wasilisho la 4a</i> na <i>Zoezi la 4.8.1: Ni kwa kiasi gani milo yetu hukamilika?</i> Mlo kamili ni nini? (<i>angalia 4.8.1</i>). [dakika. 10 na 40] | <ul style="list-style-type: none"> - Chati mgeuzo, kalamu za wino mnene, gundi ya utepe, vibandiko vya kushikia. - <i>Zoezi la 4.8.1: Wasilisho la 4a</i> chati mgeuzo, kalamu na gundi ya utepe. |

| | | <ul style="list-style-type: none"> - Kujua namna viazi vitamu lishe rangi ya chungwa vinavyopunguza upungufu wa vitamini A. - Kuwa na uwezo wa kuandaa mlo wa viazi vitamu lishe rangi ya chungwa utakaokuwa karibu na rafiki zaidi kwa watoto. - Kuelewa umuhimu wa kuzingatia mambo ya jinsia juu ya lishe katika hatua ya kaya. | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 4b</i> na Zoezi la 4.8.2: <i>Kula mlo wenye vitamini A kwa wingi</i>. Kwa nini viazi vitamu lishe rangi ya chungwa vinasaidia kudhibiti upungufu wa vitamini A na nani wako katika hatari ya upungufu wa vitamini A (<i>angalia 4.8.2</i>. [dakika 10 na 20]) - Zoezi la 4.8.3: <i>Uandaaji wa uji (angalia 4.8.3)</i>. {<i>Angalizo: Uandaaji wa uji hufanyika Siku ya 1; vyakula vingine vya viazi vitamu lishe rangi ya chungwa huandaliwa Siku ya 9</i>}. [saa 1] - Zoezi la 4.8.4: <i>Kukuza uelewa na kujenga mahitaji ya viazi vitamu lishe rangi ya chungwa (angalia 4.8.4)</i>. [dakika 55] - <i>Mjadala katika vikundi juu ya uimara na udhaifu wa mbinu na zana zinazotumika</i>. Hivi kweli tunajumuisha jinsia kisawasawa? [dakika 30] | <ul style="list-style-type: none"> - Zoezi la 4.8.2: <i>Wasilisho la 4b</i>, karatasi zenye ukubwa wa A4 na kalamu, mifano halisi ya vyakula vya asili vyenye vitamini A kwa wingi ikiwemo maboga, mapapai, vitamu lishe rangi ya chungwa, mbogamboga za majani za asili na zile zisizo za asili, na kadhalika kama zinapatikana. - Zoezi la 4.8.3: 4: Seti za kadi za mfano wa uji mzito zenye picha na maelezo ya viambato ambavyo vinaweza kutumika kutengeneza uji wa lishe wa mtoto. (Kitini cha 4.8.3a). - Zoezi la 4.8.4: Mada ya 4 ya Kitabu cha Wakufunzi. |
|------|--|---|--|--|
| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/ Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
| 4 | Kuchagua, kutunza na kuzalisha vipando vya viazi vitamu. | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuwa na uwezo wa kutaja/kutambua, kuchagua na kutunza vifaa safi vya kupandia viazi vitamu. - Kufahamu kuhusu kanuni za uchaguzi mzuri na utunzaji wa vipando. - Kuelewa namna ya | <ul style="list-style-type: none"> - Zoezi la 5.10.1: <i>Miche kwa ajili ya kupandikiza: Salama na iliyozalishwa</i>: Kazi/shughuli ya shamba kubaini vipando salama, uchukuaji vipandikizi vya miche, vikate viwe vipando, jifunze namna ya kupanda kwa wingi na kwa kasi kubwa katika kijaruba, mjadili namna ya kuvitunza, lini na namna ya kupandikiza, kokotoa kiwango cha kuzaliana kwa miche. [saa 2 na dakika 5] - <i>Wasilisho la 5a</i> kuhusu vipando vya viazi | <ul style="list-style-type: none"> - Zoezi la 5.10.1: Eneo jirani lililopandwa viazi vitamu likiwa na baadhi ya mimea ya viazi vitamu iliyoathiriwa na virusi, nusu ya kitalu kilicho kamilika tayari, visu vitano vya kukatia, galoni mbili za kumwagilia zikiwa na maji ndani yake, na majembe ya mkono mawili. - Wasilisho la mada juu ya vifaa au nyenzo. Shamba la uzalishaji haraka la karibu lililopandwa wiki 8 kabla ya kuanza kwa mafunzo, aina mbili ya viazi vitamu vyenye viwango tofauti vya uzaaji. Chati mgeuzo, |

| | | | | |
|--|--|--|---|--|
| | | <p>kukokotoa viwango vya uzalishaji miche na kwa vipi viwango vya aina mbalimbali hutofautiana</p> | <p>vitamu, michakato ya kiasilia ya utunzaji, usimamizi wa matumizi [umwagiliaji wa matone] kunyunyizia), mfumo wa 'S' Tatu, na mahema ya wavu.</p> <ul style="list-style-type: none"> - Mjadala: Mifumo iliyopo ya mbegu ya 'S' Tatu. [dakika 20] - <i>Zoezi la 5.10.2: Mfumo wa S Tatu</i> Kuifanyia majaribio kwa vitendo njia ya 'S' Tatu, kuanzia ile hatua ya kuchagua viazi, kupakia na kubadilisha katika eneo kavu lenye ubaridi. [saa 1 na dakika 30] - <i>Mazoezi ya ziada:</i> Kama muda unaruhusu, tengeneza hema la wavu (angalia Kiambatanisho cha 5.2) au fanya majaribio ya kuimarisha miche iliyozalishwa kwa njia ya tishu (angalia Kiambatanisho cha 5.1). | <p>kalamu ya wino.</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 5a</i> juu ya vipando. - <i>Zoezi la 5.10.2:</i> Viazi vitamu karibu ya 200 vikiwemo baadhi vilivyoharibiwa kabisa, beseni 6, magazeti, ndoo 5, fagio 5. Tengeneza mfumo mmoja wa 'S' Tatu miezi 3 kabla ya kozi ya mafunzo kwa wakufunzi kuanza ili wanafunzi wajionee wenyewe mizizi inavyochipua au kuharibiwa. <p><u>Maandalizi ya awali:</u></p> <ul style="list-style-type: none"> <i>Kwa Zoezi la 5.10.1:</i> Fanya maandalizi na mmiliki wa shamba kwa ajili ya washiriki kutembelea, kuchagua na kukata vikonyo vya mashina dhaifu. Lazima liwe shamba lenye virusi na lina matatizo ya kuathiriwa na fukusi wa viazi vitamu, na baadaye washiriki watafanya mazoezi ya uchaguzi ulio bora zaidi kwa vitendo. • Andaa kitalu cha uzalishaji haraka wiki 8 kabla ya mafunzo kilichopandwa aina mbili za viazi vitamu zenye viwango tofauti vya uzaaji (mfano mita moja ya mraba (vipando 50) vya Aina A, na mita moja ya mraba (vipando 50) vya Aina B. • Andaa nusu ya kitalu cha uzalishaji haraka shambani, ambacho washiriki wanaweza kukimalizia na kisha kufanya majaribio ya kupandikiza vipando walivyovipata, kuwekea kivuli na kumwaglia. • <i>Kwa Zoezi la 5.10.2:</i> Weka Mfumo wa 'S' Tatu kwa miezi michache kabla ya kuanza mafunzo ya wakufunzi ili wanafunzi waweze kuchimbua viazi na kuangalia vikianza |
|--|--|--|---|--|

| | | | | <p>kuchipua ambapo wanaweza kufanyia majaribio ya kupandikiza tena.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kama unakusudia kujumuisha mazoezi ya vitendo kwenye ujenzi wa hema la wavu au uimarishaji kutumia vijimea vilivyokuzwa kwa tishu, matayarisho ya mapema yatahitajika (angalia Kiambatanisho cha 5.1 na 5.2). |
|------|--|--|---|--|
| Siku | Mada | Matokeo ya kujifunza yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
| 5 | Wadudu waharibifu na magonjwa yanayoathiri viazi vitamu na namna ya kuyadhibiti. | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuwa na uwezo wa kutafuta mifano ya wadudu waharibifu na magonjwa yanayoathiri viazi vitamu na kuelezea na kuonyesha madhara yanayosababishwa na kila mdudu na ugonjwa. - Kufahamu kiwango cha mbinu za vitendo za kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa makuu ya viazi vitamu. | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 7.9.1:</i> Uwindaji wa wadudu waharibifu na magonjwa ya viazi vitamu shambani na kujifunza namna ya kudhibiti, ukusanyaji wa viazi vilivyoharibiwa na majani au matawi yenye ugonjwa, uchunguzi wa wadudu waharibifu katika shamba la viazi vitamu, mjadala wa vikundi na kuchangiana mawazo kuhusu wapi wadudu na magonjwa yanakotokea na namna yanavyosambaa kwa kasi (ukihusisha nzi weupe kama inawezekana). Husisha mazoezi kwa vitendo na kujadili namna ya kuponya na kuondoa mimea ya viazi vitamu iliyoathirika na virusi vya magonjwa ya viazi vitamu (angalia Zoezi la 7.9.1). [dakika 85] - <i>Wasilisho la 7a:</i> Mzunguko wa maisha ya wadudu, na magonjwa makuu ya viazi vitamu. [dakika 30] - <i>Zoezi la 7.9.2: Uharibifu uliofichika:</i> Kuchanganua na kupasua viazi | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 7.9.1:</i> Ni bora kuwa na zao changa jirani lenye magonjwa ya virusi vya viazi vitamu, kwenye shamba ambalo hapo awali lilikuwa na mazao ya viazi vitamu na lenye viazi vilivyokomaa au vilivyokaa muda mrefu ili kwamba washiriki waweze kufanyia utafiti na kutafuta magonjwa na miche ya viazi vitamu iliyoharibiwa na wadudu; fimbo 20 za kuchimbia; mifuko 8; vifaa au majagi au mabeseni angavu 20 yenye mifuniko na tundu chache; lensi mkuzo 20; washiriki wabebe madaftari yao na penseli; chati mgeuzo na stendi zake; kalamu za wino mnene pamoja na gundi ya utepe. - <i>Wasilisho la 7a:</i> Mzunguko wa maisha wa wadudu waharibifu na magonjwa makuu ya viazi vitamu. - <i>Zoezi la 7.9.2:</i> Viazi vitamu 50 vilivyoharibiwa na fukusi; mbao 20; visu vikali 20; lensi mkuzo 20; mabeseni au mifuko ya plastiki 40; seti moja ya mizani kwa ajili ya kupimia baadhi ya |

| | | | | |
|--|--|--|---|---|
| | | | <p>vilivyoathirika ili kubaini hatua mbalimbali za mzunguko wa maisha ya fukusi aina ya 'Cylas' na kukokotoa asilimia ya viazi iliyoharibiwa kabisa na fukusi. (Angalizo: Mwezesaji atayarisha viazi vitamu vilivyoathiriwa na fukusi mapema [angalia 7.9.2] [saa 1]</p> <p><i>Wasilisho la 7b:</i> Kuwasilisha na kujadili kuhusu namna ya kusimamia kwa vitendo uhibitwa wa wadudu waharibifu na magonjwa yanayoshambulia viazi vitamu (pamoja na panya fuko). [dakika 45]</p> <p>- <i>Zoezi la 7.9.3: Kuwafundisha wengine kuhusu wadudu waharibifu na magonjwa ya viazi vitamu:</i> Uandaaji wa mawasilisho na mazoezi kuhusu safu ndefu ya wadudu waharibifu na magonjwa makuu ya viazi vitamu (angalia 7.9.3). [saa 1 dakika 45]</p> | <p>viazi vitamu vilivyoharibiwa na vile ambavyo havijaharibika; madaftari na penseli kwa ajili ya washiriki kutumia.</p> <p>- <i>Wasilisho la 7b</i> kuhusu taratibu za uhibitwa wa wadudu waharibifu na magonjwa ya viazi vitamu.</p> <p>- <i>Zoezi la 7.9.3:</i> Viazi, vipando na wadudu vilivyokusanywa wakati wa msako kule shambani asubuhi ile; chati mgeuzo, kalamu 40 za wino mnene, gundi ya utepe, lensi-mkuzo, paketi 3 za vibandiko, madaftari na peni kwa ajili ya washiriki.</p> <p><i>Maandalizi ya awali:</i> <i>Kwa Zoezi la 7.9.1:</i> Bainisha mashamba kadhaa ya karibu (moja lenye mazao machanga yenye virusi vya magonjwa ya viazi vitamu, na mengine ambayo hapo awali yalipandwa viazi vitamu na yenye viazi vitamu vilivyokomaa au viazi vitamu vilivyozeeka) ambavyo washiriki watawachunguza na kubaini mimea ya viazi vitamu yenye magonjwa na wadudu waharibifu wa viazi vitamu. <i>Kwa Zoezi la 7.9.2:</i> Kusanya viazi vitamu vilivyoharibiwa na wadudu wiki kadhaa kabla ya kuanza kwa mafunzo. Washiriki wanaweza kuvipata baadhi wakati wa utafutaji shambani ila kama hawavipati, mwezesaji lazima awe na hakika kuwa wanavyo kiasi fulani kwa ajili ya kuvikata ili kuangalia mayai, viluilui, mabuu na vishimo vya kupatia chakula. Hii inaweza kuhitaji kutafuta viazi vya bandia vya maabara kama vile vya shambani havipatikani kwa urahisi wakati wa mafunzo.</p> |
|--|--|--|---|---|

| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
|------|--|---|---|---|
| 6 | Uzalishaji wa viazi vitamu na usimamizi wa mazao | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kusaidia wakulima kufanya majaribio katika mashamba yao ya kulinganisha aina nyingi mbalimbali za viazi vitamu au taratibu mbalimbali za usimamizi. - Kuelewa hatua mbalimbali za mzunguko wa zao la viazi vitamu na jinsi ya kusimamia kila hatua | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 6.9.1:</i> Ulinganisho wa aina mbalimbali za viazi vitamu na taratibu za usimamiaji wa viazi vitamu. Kuandaa shamba darasa la majaribio ya viazi vitamu. (angalia maelezo katika 6.9.1). [saa 3] - <i>Zoezi la 6.9.2:</i> Maandalizi ya awali: Kuandaa kalenda ya kilimo cha viazi vitamu na kutambua maandalizi ya awali na shughuli za usimamizi wa mazao hayo. Pia kufanya mijadala juu ya majukumu ya kijinsia yanayohusiana na shughuli hizi na kuangalia mabadiliko yanayojitokeza. (angalia 6.8.1). [dakika 75] - <i>Wasilisho la 6:</i> Mzunguko wa maisha ya zao la viazi vitamu (ukijumuisha hatua za baada ya kuvuna): Washiriki watachora ule mzunguko wa zao katika madaftari yao, na baada ya mjadala kuongeza maelezo ya kina juu ya nini kiangaliwe kwa makini zaidi katika kila hatua. [dakika 45] | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 6.9.1:</i> Chati mgeuzo, kalamu ya kuwekea alama, gundi ya kuzungushia, sepeto, karatasi za kuandikia vitambulisho, vijiti, shamba jirani la kufanyia majaribio, Mada ya 3, 6 na 7 ya Kozi ya Wakufunzi, kurasa za 20-22 za kitini 'Ni nini kinachoniharibia viazi vitamu? - <i>Zoezi la 6.9.2:</i> Chati mgeuzo, kalamu za wino mnene, penseli, gundi ya utepe. - <i>Wasilisho la 6</i> hatua za ukuaji wa viazi vitamu na shughuli za usimamizi zinazohitajika. <u><i>Maandalizi ya awali:</i></u> <i>Kwa zoezi la 6.9.1:</i> Bainisha shamba la karibu <u><i>la ukubwa wa mita 30</i></u> kwa 30 ambalo washiriki wanaweza kutumia kuandaa na kufanya majaribio. |
| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
| 7 | Kupanga programu ya usambazaji wa vipando | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuelewa hatua zote za msingi na vikwazo vinavyoweza kujitokeza | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 5b:</i> Kanuni muhimu za kuzalisha na kusambaza vipando vya viazi vitamu. [dakika 30] - <i>Zoezi la 5.10.3: Mkakati wa kupanga</i> | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 5b</i> kuhusu kanuni muhimu. - <i>Zoezi la 5.10.3:</i> Chati mgeuzo na kalamu za wino mnene; nakala 35 tupu za kalenda ya shughuli za viazi vitamu (Kitini cha 5.10.3a); |

| | | | | |
|-------------|-------------|--|--|--|
| | | <p>wakati wa kupanga uzalishaji kwa wingi au kutumia mchakato wa DVM wa usambazaji.</p> <ul style="list-style-type: none"> - Kufanya zoezi la kuandaa programu ya usambazaji wa vipando katika eneo lao vitakavyofikia kaya 5,000 - Kuelewa ni kwa nini ni muhimu kufuatilia na kutathmini miradi. - Kufanya zoezi la kufuatilia usambazaji wa vipando na pembejeo. | <p><i>kuzalisha na kusambaza vipando: Zoezi la vitendo. [saa 3]</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Mijadala ya vikundi:</i> Kulinganisha mikakati ya mazingira mbalimbali yanayo husiana na kilimo cha viazi vitamu. [dakika 20] - <i>Zoezi la 5.10.4:</i> Kufanya kazi na DVM. Zoezi la vitendo. [saa 2.5] - <i>Wasilisho 5c:</i> Kutayarisha gharama za zoezi zima la usambazaji wa vipando vya viazi vitamu. [dakika 10] - <i>Wasilisho la 12.</i> Kutambulisha U na T. [dakika 20] - <i>Zoezi la 12.7.1: Imeenda wapi?</i> Fanya zoezi la kufuatilia usambazaji wa vipando. [dakika 30] - <i>Kazi ya nyumbani:</i> Kutafuta gharama za mkakati wa usambazaji. | <p>nakala 35 tupu za kufanyia kazi za kukokotolea mkakati wa uzalishaji viazi vitamu (Kitini cha 5.10.3b); nakala 35 tupu za kufanyia kazi za mfano wa mkakati wa usambazaji viazi vitamu (Kitini cha 5.10.3c).</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 5.10.4:</i> Kitaru cha majaribio kilicho jirani kilichopandwa aina mbili tofauti za viazi vitamu zilizotenganishwa, kuwekwa alama na zina vipando safi na kitalu cha pili chenye mchanganyiko wa vipando/miche iliyoathiriwa na isiyoathiriwa. Pia mchanganyiko wa aina mbalimbali za viazi vitamu zinazohitajika kwa ajili ya mafunzo; chati mgeuzo; kalamu za wino mnene; gundi ya utepe, nakala za nukuu za kitini cha 5. 10.4a na 5.10.3b. - <i>Wasilisho la 5c</i> juu ya gharama za uzalishaji na usambazaji wa viazi vitamu. - <i>Wasilisho la 12:</i> kutambulisha U na T. - <i>Zoezi la 12.7.1:</i> Vocha 200 za vipando zilizojazwa zenye taarifa inayohitajika kwa ajili ya Jedwali la 12.5.2. nakala 40 za fomu ya 12.5.2, kalamu. <p><i>Maandalizi ya awali: Kwa Zoezi la 5.10.4:</i> Bainisha au panda aina mbili kwenye vitaru vilivyo jirani katika hali tofauti kwa kila kitaru. Tenganisha miche ili kuweza kuondoa ile yenye magonjwa halafu uache kitaru kingine kwa majaribio kwa matumaini kwamba athari za virusi na dalili zitaonekana.</p> <p><i>Kwa Zoezi la 12.7.1:</i> Kusanya au jaza vocha 200 za vipando zilizokamilika.</p> |
| Siku | Mada | Matarajio ya somo | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |

| | | yaliyokusudiwa | | |
|---|---|--|--|---|
| 8 | Uvunaji, usindikaji na usimamizi baada ya mavuno. | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kufahamu kuhusu mambo makuu ya uvunaji, usimamizi na usindikaji baada ya mavuno. - Kuelewa ni vipi usindikaji na uhifadhi wa viazi vitamu lishe unaathiri kiwango cha vyanzo vya vitamini A. - Kuelewa umuhimu wa kuhusisha makundi mbalimbali katika mchakato wa mafunzo na uhamasishaji. | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 8.9.1: Kuongeza faida kupitia uhifadhi wa viazi vitamu vibichi.</i> Mazoezi ya shamba ya kuvuna viazi, kutenga viazi vibovu, kutengeneza ghala la shimo la kuhifadhia viazi (majani, nguzo za mianzi na mbao kwa ajili ya kufunikia linapashwa liandaliwe mapema na mashimo kuchimbwa mapema (angalia 8.9.1) [saa 2] - <i>Zoezi la 8.9.2: Athari ya kukausha kwa jua na kuhifadhi kwenye viwango vya vyanzo vya vitamini A vya viazi vitamu lishe.</i> Washiriki waweke sampuli tatu za chipsi za viazi vitamu lishe zilizokaushwa kwa kutumia jua kwa muda wa siku 7, 5, au 2 ili washiriki watazame kwa kuchunguza tofauti zilizopo baina ya sampuli hizo, hasa wazingatia utofauti wa rangi. Ikiwezekana, wape beta-karotini kwa kadirio la kila sampuli tofauti. (angalia zoezi la 8.9.2 [dakika 30]) - <i>Wasilisho la 8.</i> Wasilisha mada itakayohusu uvunaji kidogokidogo wa zao lililokomaa, ukaushaji wa viazi vitamu vilivyokatwa vipande vidogovidogo na kuvitandaza kwenye vichanja; lakini wakati wakufanya kazi hizi zote ni muhimu kuzingatia suala la jinsia. Usimamizi wa baada ya mavuno wa viazi vitamu vibichi na chipsi zilizokaushwa; vifaa vya kuwekea, | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 8.9.1:</i> Shamba la viazi vitamu la karibu lililotayari kuvunwa na; ambalo washiriki wanaweza kuchimba mimea hadi 10 kwa kikundi ili kutafuta kiwango cha mavuno, mizani, magunia; kikokotoo; kalamu na karatasi; chepeo; majembe; nyasi kavu; nguzo za mianzi; fimbo za kuvunia; matawi, kamba na nyasi za kuelekea. - <i>Zoezi la 8.9.2:</i> Viazi vitamu vibichi 50 rangi ya chungwa, mashine ya kukatia, kichanja cha kuanikia, angalau mabe mikoba mitatu ya sampuli, lebo/kitambulishi, kalamu za wino mnene, seti ya taarifa inayoonyesha yaliyomo ndani ya karotini na namna karotini inavyopungua kutokana na jua linavyoendelea kukausha, nakala za kutosha za seti ya taarifa zinazoonyesha pia namna ambavyo karotini inapungua kutokana na uhifadhi wa muda mrefu sana wa viazi ndani ya ghala. (Kitini cha 8.9.2a) - <i>Wasilisho la 8:</i> Wasilisha mada inayohusu zaidi uvunaji, ukaushaji, usagaji na masuala yanayohusu jinsia baada ya kuvuna. - <i>Zoezi la 9.8.1:</i> inaonyesha vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kundi dogo tu: Kikaangio; mkaa au jiko la stovu; ubao kwa ajili ya kukatia; lita moja ya maji ya vuguvugu; kikandio; kifaa cha kukamulia matunda; chombo cha kuhifadhia chakula; bakuli; sahani; visu; kilo mbili za unga wa ngano; nusu kilo ya viazi vitamu lishe; nusu kilo ya viazi vitamu lishe vilivyochemshwa; |

| | | | | |
|--|--|--|---|--|
| | | | <p>kukinga wadudu na ufuatiliaji wa muda. Uliza katika kaya ni nani anahusika na uhifadhi, na jinsi ujumbe huu utakavyowafikia. [dakika 45]</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 9.8.1: Kutumia unga wa viazi vitamu badala ya unga wa ngano kupikia chapati na Zoezi la 9.8.2: Kutengeneza juisi ya viazi vitamu na Zoezi la 9.8.3 kutengeneza fiosis za viazi vitamu. Wagawe washiriki katika makundi mawili na kisha katika vikundi vidogo halafu waambiwe wafanye zoezi la 9.8.1 au (9.8.2 na 9.8.3). [saa 2 na dakika 30]</i> - <i>Wasilisho la 9: Usindikaji na mjadala kuhusu nani alengwe kwenye mafunzo ya usindikaji, watu kama wasindikaji wadogo na wanaoweza kutumia viazi vitamu lishe kwenye shughuli zao. Mijadala kuhusu umuhimu wa kuhusisha wanaume japokuwa wanawake ndio watayarishaji wa chakula, lakini wanaume bado wana ushawishi kuhusu ni chakula gani kipandwe au kinunuliwe. [dakika 45]</i> | <p>nusu kilo ya unga wa viazi vitamu lishe; kikombe kimoja cha mafuta ya kupikia mboga za majani; chumvi; chati mgeuzo; kalamu za wino mnene na gundi ya utepe.</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 9.8.2: Vikombe vinne vya sukari; viazi 8 vilivyochemshwa; vijiko vitatu vya asidi ya limau au juisi inayotokana na matunda 5; lita 5 za maji yaliyochemshwa na kupoa; kwa kuweka ladha ongeza ukwaju, tunda la pasheni, nanasi au juisi ya chungwa; kikamulio cha matundu, kijiko cha mbao, majagi matano; chupa safi za ujazo wa lita moja; weka juisi yote kwenye jokofu.</i> - <i>Zoezi la 9.8.3: Gramu 300 (vikombe 2–2½) unga wa ngano; jibini gramu 50; gramu 200 (kikombe 1–1½) rojo ya viazi vitamu; gramu 65 (kikombe ¼) sukari; mayai 2; mafuta ya kukaangia; hamira vijiko 2 vya chai; bakuli la kuchanganyia, kijiko cha mbao, sufuria, chekeche, kikaangio, bakuli.</i> - <i>Wasilisho la 9: Kuhusu usindikaji na nani wa kumhusisha kwenye mafunzo ya usindikaji, na masuala ya kijinsia.</i> <i>Maandalizi ya awali:</i> <ul style="list-style-type: none"> • <i>Kwa Zoezi la 8.9.1. Bainisha au panda kiunga cha viazi vitamu ambacho wakufunzi wanaweza kuvuna ili kukokotoa mavuno.</i> • <i>Kwa Zoezi la 8.9.2. Siku ya kwanza kati ya siku 10 za mafunzo/kozi ya mafunzo kwa wakufunzi, andaa kiasi kidogo cha chipsi za viazi vitamu lishe na mahali ambako kuna vichanja kwa ajili ya ukaushaji kwa kutumia jua (ukaushaji kwa kutumia jua utafanyika</i> |
|--|--|--|---|--|

| | | | | <p>kwa siku 7 kwa sampuli), siku ya 3 ongeza kiwango cha viazi vitamu lishe kwenye vichanja vile lakini usichanganye na sampuli ya awali. Hakikisha sampuli zote zimewekwa alama za kutambulisha na ziko salama. Siku ya 6, ongeza tena kiasi cha ziada cha viazi vitamu lishe na kuviweka katika ngazi ya juu ili kukausha kwa jua, ila hakikisha alama ya kutambulisha imewekwa vizuri na havikuchanganywa na sampuli za awali. Siku ya 9 kusanya sampuli 3 (lakini hakikisha unazitenganisha) halafu zichukue sampuli zote na uzipeleke kwenye chumba cha mafunzo.</p> <ul style="list-style-type: none"> • <i>Kwa Zoezi la 9.8.1.</i> Jitahidi upate viazi vitamu lishe rangi ya chungwa vya kutosha ili kila kundi moja dogo lipate nusu kilo ya viazi hivyo. Ikiwa muda utakuwa mfupi sana, chemsha kwanza viazi vitamu lishe halafu washiriki watachuja na kuchanganya katika mlo. • <i>Kwa Zoezi la 9.8.2 na 9.8.3.</i> panga viambato vya kupikia, zana na vifaa. Pata viazi vitamu lishe vya kutosha. Muda ukiwa hauruhusu vichemshe viazi vitamu lishe mapema ili washiriki waweze kuviponda tu na kuvitumia kwenye mapishi. |
|------|-------------------------|--|--|---|
| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
| 9 | Masoko na ujasiriamali. | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuwa na uelewa kuhusu dhana ya | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 10.10.1: Ziara ya sokoni.</i> Ziara ya kutafiti sokoni ambayo nusu ya washiriki watashughulika na faida za kutafuta soko | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 10.10.1:</i> Soko lililo jirani, usafiri, vikombe 5, vyombo 5 vya plastiki (kilo 2 za viazi vitamu kwa mujibu wa uwezo), madaftari |

| | | | | |
|--|--|---|--|--|
| | | <p>utafutaji masoko na mwelekeo wa soko.</p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuelewa nguzo kuu tano na utafutaji, upatikanaji soko na uuzaji wa mazao. - Kuelewa fursa na changamoto zilizopo katika soko na uuzaji wa viazi vitamu lishe vilivyosindikwa. - Kuwa na uzoefu na ufahamu mkubwa wa namna ya kuelimisha wafanyabiashara wa zao hili. - Kuwa na uelewa makini wa namna ya kuchagua mchakato sahihi unaofaa kwa kuiandaa na kuiweka vizuri bidhaa tayari kuingizwa sokoni. - Kufahamu namna ya kufanya hesabu ya kupata soko la uuzaji wa zao jipya ambalo bado liko safi sana na tayari mchakato wa zao hilo umeshafanyika vyema - Kufahamu namna ya kufanya hesabu ya | <p>la viazi vitamu na masuala mengine na nusu nyingine watashughulika na bidhaa za kusindika, kuangalia sifa na vikwazo vikiwemo masuala ya jinsia. Baada ya kurudi kwenye kituo cha mafunzo, makundi yatatoa muhtasari wa matokeo kwa kuwasilisha ikifuatiwa na mijadala (angalia 10.10.1). [saa 4 na dakika 30]</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 10a</i>. Utafutaji soko na ujasiriamali na masuala muhimu ya jinsia. Utafutaji soko kwa vikundi. [dakika 20] - <i>Zoezi la 10.10.2</i>: Kukokotoa faida. <i>Wakitumia kisa mkasa cha mkulima, washiriki watatafuta faida katika kila hatua ya mnyororo wa thamani (angalia Zoezi la 10.10.2)</i>. [dakika 45] - <i>Zoezi la 10.10.3</i>: <i>Nguzo kuu 5 za utafutaji soko</i>. Maigizo kuwafanya washiriki kugundua masuala ya utafutaji soko (angalia 10.10.3). [dakika 55] - <i>Wasilisho la 10b</i>: Nguzo kuu 5 za utafutaji soko na namna ya kuchagua bidhaa yako. [dakika 20] | <p>na kalamu, chati mgeuzo na vifaa vya kuwekea alama.</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 10a</i> juu ya masoko na ujasiriamali na masuala muhimu ya jinsia. - <i>Zoezi la 10.10.2</i>: Nakala za kutosha za Kisa Mkasa cha Esther (Kisanduku cha 10.3). - <i>Zoezi la 10.10.3</i>: Viazi vitamu lishe rangi ya chungwa 20, vibandiko na gundi, kalamu zenye wino mnene, chati mgeuzo, gundi ya utepe.. - <i>Wasilisho la 10b</i> kuhusu nguzo tano za masoko na namna ya kuchagua bidhaa yako. <p><i>Maandalizi ya awali:</i> <i>Kwa Zoezi la 10.10.1</i>: Fanya mipango ya usafiri, kabla ya biashara ya kuuza viazi vitamu kufanyika. Mwezesaji anapaswa kutembelea eneo la soko ili kutafuta mahali waliko wanunuzi wa viazi vitamu na kuangalia endapo bidhaa zinazotokana na kusindikwa ziko sokoni zinauzwa, na kama haziko, wataangalia ni bidhaa gani zilizosindikwa zinaweza kuwafanya washiriki kujifunza kitu fulani.</p> |
|--|--|---|--|--|

| | | kupata soko la uuzaji wa bidhaa ambayo imeisha pitia mchakato wa kutoka katika hali ya unga kuwa uji mzito. | | |
|------|--|---|--|--|
| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
| 10 | Mpango wa kuwafunza watu wengine juu ya 'Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu'. | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kufahamu na kuandaa rasimu ya matokeo ya mafunzo na mbinu, vifaa vya mafunzo na kuandika mipango na mikakati (muda, mahali na eneo la utafiti, washiriki) wa kozi ya mafunzo ya viazi vitamu waliyokuwa wanaitoa - Kuwa na uwezo wa kutoa mafunzo kwa vitendo kwa muda wa siku 5 za 'Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu'. | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 1.4.1:</i> Mazoezi ya kuwa mwezesaji wa kujifunza kwa vitendo. Fanya mazoezi ya uwezesaji katika mada kuu ya viazi vitamu na kufanya kazi kwa vikundi kuangalia kanuni za kutoa na kupokea mrejesho unaojenga (<i>angalia Zoezi la 1.4.1</i>). [saa 2 na dakika 30] - <i>Wasilisho la 1:</i> Kuwasaidia wazee kujifunza na kuelewa programu inayoshauriwa ya siku 5 ya mafunzo ya wakufunzi (angalia Mada ya 13. Mjadala kuhusu, na kuandaa utaratibu wa mpango wa kuwasilisha (angalia Kiambatanisho cha 1.3). [saa 1] - <i>Zoezi la 1.4.2:</i> Mawazo kuhusu shughuli za ziada za viazi vitamu za kujifunza kwa vitendo (angalia Zoezi la 1.4.2). [saa 1 na dakika 20] - <i>Zoezi la 1.4.3:</i> Kutathmini kozi ya mafunzo: Tathmini ya kozi (angalia Zoezi la 1.4.3) (<i>Chaguo la kurudia zoezi la ufahamu wa</i> | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 1.4.1:</i> Kadi za mada kuu kutoka katika kozi ya siku 5 ya Mafunzo ya Wakufunzi, washiriki wanahitaji kitabu chao cha 'Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu', madaftari na peni; vibandiko, chati mgeuzo, gundi ya utepe, kalamu za wino mnene, zana zote zilizotumika wakati wa programu ya mafunzo ikiwemo viazi vitamu 100 baadhi yake vikiwemo viazi vitamu lishe rangi ya chungwa. - <i>Wasilisho la 1:</i> Kuwasaidia watu wazima kujifunza na programu ya kozi ya siku 5 ya Mafunzo kwa Wakufunzi (angalia Mada ya 13). - <i>Zoezi la 1.4.2:</i> Washiriki wanahitaji kitabu chao, madaftari na kalamu; vibandiko, chati mgeuzo, gundi ya utepe, kalamu za kuwekea alama, zana zote zilizotumika wakati wa programu ya mafunzo ikiwemo viazi vitamu 100 baadhi yake vikiwemo viazi vitamu lishe rangi ya chungwa. |

| | | | | |
|--|--|--|--|--|
| | | | <p>viazi vitamu kama zoezi la kutokea (Kiambatanisho cha 1.2). [saa 1].</p> <p>- Utoaji vyeti. [saa 1]</p> | <p>- Zoezi la 1.4.3: Nakala za kutosha za fomu ya 12.5.5c za tathmini ya kozi kwa kila mshiriki, kalamu, nakala za kutosha za jaribio la ufahamu wa viazi vitamu (Kiambatanisho cha 1.2) kama unapanga kufanya jaribio lililopo.</p> <p>- Vyeti vilivyokamilishwa, vinywaji.</p> |
|--|--|--|--|--|

Jedwali la 13.2: Maandalizi ya awali yanayohitajika katika kozi ya siku 10 ya mafuzo kwa wakufunzi

| Maandalizi ya awali: | Ratiba kuhusu muda unaoshauriwa wa matayarisho ya awali kabla ya kuanza kwa Kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi | | | | | | |
|--|--|--------------------|---------------|---------------|---------------|---------------|--------------|
| | Miezi 6 kabla | Miezi 5 kabla | Miezi 4 kabla | Miezi 3 kabla | Miezi 2 kabla | Mwezi 1 kabla | Wiki 1 kabla |
| Kuchagua na kuwasiliana na wawezeshaji | — | — | — | — | — | — | — |
| Kutangaza Kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi | — | — | — | — | — | — | — |
| Kupanga matayarisho eneo la kazi yanayohitajiwa (angalia orodha hapa chini) | — | — | — | — | — | — | — |
| <i>Zoezi la 3.5.1: Tambua tofauti.</i> Bainisha au panda shamba la karibu (jirani na kituo cha mafunzo) aina mbalimbali za viazi vitamu, baadhi ya viazi hivi na majani viweze kuvunwa na washiriki wakati wa mafunzo. Kutana na wakulima ili kujadili na kupanga. | — | Pandikiza au panga | — | Fuatilia | — | Fuatilia | Fuatilia |
| <i>Zoezi la 5.10.1: Miche ya kupanda; Salama na iliyozaliana.</i> Bainisha shamba la karibu ambalo lina uwezekano wa kuwa na matatizo ya virusi na wadudu waharibifu wakati wa Kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi, na ambapo washiriki wanaweza kupata miche ya vipandikizi. | — | — | — | Bainisha | — | Fuatilia | Fuatilia |
| <i>Zoezi la 5.10.1:</i> Andaa eneo jirani la kuzalishia kwa haraka lililopandikizwa vipandikizi aina mbili zinazotofautiana sana katika viwango vya uzalianaji (mfano, mita ya mraba mmoja vipandikizi 50) vya Aina A, na mita ya mraba mmoja vipandikizi 50 vya Aina B. Washiriki watawuna vipando. | — | — | — | Tafuta eneo | Andaa | Fuatilia | Fuatilia |

| | | | | | | | |
|--|---|--------------------|---|------------------|-------|----------------|----------|
| Zoezi la 5.10.1: Tayarisha nusu ya kitaru cha kuzalishia shambani, ambacho washiriki watakimalizia na kufanya mazoezi ya kupandikiza vipando walivyovipata, kuwekea kivuli na kumwagilia. | — | — | — | — | — | — | Andaa |
| Zoezi la 5.10.2: Mfumo wa S Tatu: Tengeneza mfumo wa 'S' Tatu, ambao wakati wa mafunzo washiriki wanaweza kuviona viazi vikichipua na kuweza kuvitumia katika mazoezi ya upandikizaji. | — | — | — | — | Andaa | Fuatilia | Fuatilia |
| Zoezi la 5.10.4: Kufanya kazi na DVMs: Bainisha au pandikiza vitaru viwili vya jirani aina mbili tofauti ya viazi vitamu kila kimoja. Kimojawapo king'olee miche iliyoshambuliwa na magonjwa tayari. Kiache kingine kwa matumaini kwamba maambukizi ya virusi na dalili zake vitajitokeza. | — | Pandikiza au panga | — | Ng'olea kitalu 1 | — | Fuatilia | Fuatilia |
| Mazoezi ya ziada: Kama unapanga kutengeneza hema la wavu (Kiambatanisho cha 5.2) au kufanya mazoezi ya kuimarisha vijimimea vilivyozalishwa kwa njia ya tishu (Kiambatanisho cha 5.1) utahitaji kufanya matayarisho sahihi ya awali (zana, eneo na kadhalika). | — | — | — | — | — | Panga na andaa | Fuatilia |
| Zoezi la 6.9.1: Kulinganisha aina mbalimbali za viazi vitamu na namna ya kusimamia. Tafuta eneo tupu la shamba (mita 30x30) ambapo washiriki wanaweza kufanya mazoezi ya kusanifu na kuandaa shamba darasa. | — | — | — | — | — | Bainisha | Fuatilia |

| Mandalizi ya awali: | Ratiba kuhusu muda unaoshauriwa wa matayarisho ya awali kabla ya kuanza kwa Kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi | | | | | | |
|--|--|---------------------|---------------------|---------------------|---------------------|----------------------------|----------------------|
| | 6 Miezi kabla | 5 Miezi kabla | 4 Miezi kabla | 3 Miezi kabla | 2 Miezi kabla | 1 Mwezi kabla | 1 Wiki kabla |
| <i>Zoezi la 7.9.1: Uwindaji wa wadudu na magonjwa ya viazi vitamu shambani na kujifunza namna ya kudhibiti. Tafuta mashamba matatu ya karibu ya viazi vitamu (i) yenye miche michanga yenye virusi na magonjwa, (ii) shamba ambalo lilikuwa na viazi vitamu hapo awali, (iii) shamba lenye viazi vitamu vya zamani au vilivyokomaa, ambavyo washiriki wanaweza kufanya uvumbuzi na kulinganisha magonjwa na wadudu waharibifu.</i> | --- | Pandikiza au panga | | Fuatilia | --- | Fuatilia | Fuatilia |
| <i>Zoezi la 7.9.2: Uharibifu uliofichika. Kusanya viazi 30 vilivyoshambuliwa na wadudu kisha vihifadhi kwa uangalifu ili washiriki waweze kuvichambua wakati wa Mafunzo ya Wakufunzi.</i> | --- | | --- | --- | | Kusan ya viazi | Fuatilia |
| <i>Zoezi la 8.9.1: Kuongeza faida kwa kuhifadhi viazi vitamu vibichi. Tafuta au pandikiza viazi vitamu kitau cha karibu ambacho washiriki wanaweza kuvuna ili kukokotoa mavuno.</i> | --- | Pandikiza au panga | --- | Fuatilia | | Fuatilia | Fuatilia |
| <i>Zoezi la 8.9.2: Madhara ya kukausha kwa jua kwenye viwango vya vyanzo vya vitamini A kwenye viazi vitamu lishe rangi ya chungwa. Andaa viazi vitamu lishe rangi ya chungwa na chipsi zake kama ilivyoelezewa kwenye Zoezi la 8.9.2.</i> | --- | | --- | --- | | | Andaa chipsi za OFSP |
| <i>Zoezi la 10.10.1: Ziara ya soko. Fanya ziara ya maandalizi kwenye masoko jirani ukiwa na orodha ya vitu unavyohitaji kuona ili kuamua ni soko gani litawezesha washiriki kujifunza vyema sababu zinazoathiri soko la viazi vitamu vibichi na bidhaa za kusindikwa. Andaa usafiri wa sokoni kwa ajili ya Mafunzo ya Wakufunzi.</i> | --- | | --- | --- | | Tembelea na tafuta usafiri | |
| Majibu ya mara moja kutoka kwa waandaaji na washiriki wa kozi wenye hamasa na kujumuisha mtindo wa uchunguzi wa tathmini ndogo ya mahitaji. | --- | | | | | | |
| Wawezeshaji kujifahamisha kuhusu kitabu cha mafunzo, mbinu iliyopendekezwa, mazoezi na mawasilisho na tarehe za programu ya mafunzo (inaweza kujumuishwa na mafunzo ya maandalizi). | --- | | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|-----|-----|-----|-----|-----|-----|-----|
| Ukumbusho kwa wawezeshaji wote kuhusu programu ya Mafunzo ya Wakufunzi na tarehe watakazotakiwa. | --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| Kukamilisha orodha ya washiriki wa mafunzo, na kuwatumia maelezo kuhusu programu ya mafunzo, mahali na maelekezo. | --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| Kuwapelekea wawezeshaji muhtasari wa orodha ya washiriki wa mafunzo na historia zao na mahitaji wanayofikiria. | --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| Matayarisho ya zana za kujifunza kwa vitendo, vifaa na viungo kwa Mafunzo ya Wakufunzi (angalia mstari wima wa Jedwali la 13.1 kwa maelezo zaidi. | --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| Wasiliana na wawezeshaji wote kuwakumbusha kuhusu programu ya Mafunzo ya Wakufunzi na tarehe watakazotakiwa kuwapo. | --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| Matayarisho ya vifaa vya kuandikia, mashine ya kutolea nakala, beji za majina, maandalizi ya malazi na chakula, na vyeti. | | | | | | | |

13.2: Maelezo ya jumla juu ya siku 5 za Kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi ya Vyote Unavyopaswa Kujua Kuhusu Viazi Vitamu

Inatarajiwa kwamba watumishi wa ugani katika ngazi ya wilaya na asasi za umma zisizo za kiserikali ambao wameshiriki katika siku 10 za mafunzo kwa wakufunzi, watawafunza wafanyakazi waliopo mashambani na wale walioko ndani ya taasisi zao kwa kutumia siku 5 za mafunzo kwa wakufunzi. Halafu, wale wafanyakazi waliofunzwa mashambani watawafunza wakulima moja kwa moja kwa kutumia siku 5 za kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi. Kwa hiyo, tumeendeleza muhtasari wa mafunzo kwa wakufunzi ya siku 5 ambayo inajumuisha nafasi nyingi kwa ajili ya kila mtu kujifunza pale alipo. Programu kwa ajili ya mafunzo haya imeonyeshwa hapa chini. Wawezeshaji wanaweza kuamua kuiendesha kwa siku 5 mfululizo au kuigawa katika mafungu tofauti ya mafunzo ili kwenda sawa na mzunguko wa kilimo cha mazao mrandano cha viazi vitamu. Kama una siku zaidi ya 5, tunashauri utembelee soko (Zoezi la 10.10.1) na tumia muda wako mwingi katika kuwasaidia washiriki kufanya mazoezi kwa vitendo katika kujitolea mafunzo ya mada hizi zilizopo. Tunatumaini masomo haya yatasaidia na uombe mrejesho juu ya mafunzo haya kutoka kwa washiriki (angalia Mada ya 14 kwa ajili ya tafakuri rejeshi).

Jedwali la 13.3: Programu ya siku 5 za Kozi ya mafunzo kwa wakufunzi ya 'Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu'

| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
|------|--|--|--|---|
| 1 | Utangulizi, matarajio ya washiriki, makubaliano juu ya matokeo ya mafunzo, makubaliano kuhusu matarajio ya mafunzo, mtazamo wa jumla juu ya umuhimu na matumizi ya viazi vitamu. | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuelewa programu ya mafunzo/kozi na namna inavyolenga kuwaandaa washiriki kwa ajili ya kuwafunza wengine kuhusu kilimo cha viazi vitamu. - Kufahamu kuhusu mienendo na changamoto za uzalishaji na matumizi ya viazi vitamu. - Kufahamu michakato na changamoto zinazokumba uzalishaji na matumizi ya viazi vitamu. - Kuwa na uwezo wa kuandaa mlo wa viazi vitamu. - Kuelewa namna ya kubadili viazi vitamu lishe rangi ya chungwa na bidhaa nyingine katika utengenezaji wa kawaida. - Ufahamu na umuhimu wa masuala ya jinsia katika mnyororo wote wa thamani wa viazi vitamu. | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Utangulizi:</i> Kazi za vikundi [dakika 15] - <i>Matarajio:</i> Kubadilishana mawazo na kuweka matarajio ya vikundi katika makundi (vibandiko kwa kila mtu) na kuweka sawa haya yote pamoja na matarajio ya wakufunzi na kuboresha matokeo yanayotarajiwa kadri itakavyolazimu. [dakika 30]; - Jaribio la kuingilia: Jaribio kuhusu ufahamu wa viazi vitamu mwanzoni mwa mafunzo. [dakika 30] (Kiambatanisho cha 1.2) - <i>Programu:</i> Mtazamo wa jumla wa kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi. [dakika 10] - <i>Historia na elimu ya viazi vitamu:</i> Kazi ya vikundi vidogovidogo, ufahamu wa washiriki kuhusu historia ya viazi vitamu, umuhimu wa viazi vitamu kiutamaduni, uzalishaji na mienendo ya utumiaji wa viazi hivyo, na matatizo makubwa wanayokumbana nayo wakulima [dakika 20 kwa kazi ya vikundi, ikifuatiwa na dakika 5 za wasilisho la mambo muhimu kwa kila kikundi]. - <i>Mapishi ya viazi vitamu lishe rangi ya chungwa:</i> Washiriki watengeneze chapati kwa kutumia mapishi mbalimbali yanayotumia unga wa viazi vitamu badala ya unga wa ngano (angalia Zoezi la 9.8.1) au wanaweza | <ul style="list-style-type: none"> - Chati mgeuzo, kalamu za kuwekea alama, gundi ya utepe, vibandiko/tangazo au taarifa fulani. - Nakala za jaribio la ufahamu wa kilimo cha viazi vitamu (Kiambatanisho cha 1.2). - Mtazamo wa jumla wa programu ya mafunzo (siku na mada). - <i>Zoezi la 9.8.1:</i> Kwa kila kundi dogo: sufuria; jiko la mkaa au gesi; kikaangio; ubao wa kukatia; Lita 1 ya maji ya vuguvugu yaliyochemshwa; pini ya kuviringishia, chuma cha kushikia; kikamulio cha matunda; kifaa cha kuwekea chakula; bakuli; sahani; visu; kilo 2 za unga wa ngano; nusu kilo ya viazi vitamu lishe rangi ya chungwa; nusu kilo ya viazi vitamu lishe rangi ya chungwa iliyochemshwa; nusu kilo ya unga wa viazi vitamu lishe rangi ya chungwa; kikombe kimoja cha mafuta ya kupikia ya asili ya mboga za majani; chumvi kidogo; chati mgeuzo; kalamu ya kuwekea alama; gundi ya utepe. - <i>Zoezi la 9.8.2:</i> Vikombe 4 vya sukari; viazi vitamu 8 vya ukubwa wa kati vilivyochemshwa na kupozwa; vijiko 3 vya chai vya juisi ya limau au mchanganyiko wa matunda 5, lita 5 za maji yaliyochemsha na kupozwa; ili kuongeza ladha, ongeza tunda la |

| | | | <p>kutengeneza juisi ya viazi vitamu (angalia Zoezi la 9.8.2) au wanaweza kutengeneza uji wa viazi vitamu (angalia 9.4.1) (hakikisha kuna wigo mpana wa bidhaa zinatengenezwa. [saa 2 na dakika 30]</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 2:</i> Asili na umuhimu wa kilimo cha viazi vitamu (Mada ya Pili) ikifuatiwa na mjadala wa vikundi [dakika 45] - <i>Wasilisho la 11: Jinsia na anuwai</i> na umuhimu wake kwenye shughuli za viazi vitamu (Mada ya 11) ikifuatiwa na mjadala wa vikundi [dakika 45] | <p>ukwaju, pasheni, nanasi; au juisi ya chungwa; kichujio cha matunda; sufuria, kikamulio cha matunda, kijiko cha mbao, chupa 5 safi na tupu za lita moja moja; friji kwa ajili ya kutunza juisi isiharibike; viungo na vyombo vya kupikia na vifaa na mafuta ya kuwashia moto kwa ajili ya vikundi kuandaa uji wa viazi vitamu lishe rangi ya chungwa (angalia 9.4.1).</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 2:</i> Asili na umuhimu - <i>Wasilisho la 11: Jinsia na anuwai</i> na umuhimu wake kwenye shughuli za viazi vitamu. <p><i>Maandalizi ya awali:</i> Tafuta viazi vitamu lishe rangi ya chungwa ili kila kundi lipate nusu kilo. Kama muda hautaruhusu viazi vitamu vichemshwe mapema ili washiriki waweze kuponda na kuvitumia kwenye mapishi.</p> |
|------|---|--|--|--|
| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
| 2 | Lishe na viazi vitamu lishe rangi ya chungwa. | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuelewa mlo kamili ukoje na una umuhimu gani. - Kufahamu ni vipi viazi vitamu lishe rangi ya chungwa vinaweza kuchangia kupunguza tatizo la upungufu wa vitamini A. - Kuwa na uwezo wa kuandaa mlo unaopendwa sana na watoto. - Kuelewa umuhimu wa kuzingatia | <ul style="list-style-type: none"> - Kuchangiana mawazo: Nini maana halisi ya mlo kamili? - <i>Wasilisho la 4a na Zoezi la 4.8.1: Ni kwa kiwango gani milo yetu ni kamili?</i> Lishe bora ni nini? (angalia 4.8.1. [dakika 10 na 40]) - <i>Wasilisho la 4b na Zoezi la 4.8.2:</i> Kula mlo wenye vitamini A kwa wingi. - Vitamini A, kwa nini viazi vitamu lishe rangi ya chungwa vinasaidia | <ul style="list-style-type: none"> - Chati mgeuzo, kalamu ya kuwekea alama, gundi ya utepe, vibandiko kwa ajili ya kutambulisha tangazo la bidhaa. - <i>Zoezi la 4.8.1: Wasilisho la 4a</i>, chati mgeuzo, kalamu na gundi ya utepe. - <i>Zoezi la 4.8.2: Wasilisho la 4b</i>, karatasi za A4 na kalamu za wino, mifano halisi ya vyakula vya asili vyenye vitamini A kwa wingi kama vile maboga, mapapai, viazi vitamu lishe rangi ya chungwa, |

| | | jinsia katika lishe kwa kila kaya. | <p>kupambana na upungufu wa vitamini A na ni nani yuko katika hatari ya upungufu wa vitamini A (angalia 4.8.2. [dakika 10 na 20]</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 4.8.4 Utayarishaji wa uji (angalia Zoezi la 4.8.4) [saa 1]</i> - <i>Mjadala wa vikundi:</i> Kukuza uelewa na ujengaji wa mahitaji ya viazi vitamu lishe rangi ya chungwa (angalia Zoezi la 4.8.4). [dakika 55] - <i>Mjadala wa vikundi:</i> Uimara na udhaifu wa mbinu. Je, tunajumuisha masuala ya jinsia ipasavyo? [dakika 30] | <p>mboga za majani, na kadhalika kama vinapatiakana.</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 4.8.3:</i> Seti 4 za kadi kwa ajili ya mifano ya uji zikiwa na picha na maelezo ya viungo mbalimbali vinavyoweza kutumika kutengeneza uji wa mtoto wenye virutubisho (Kitini cha 4.8.3.a). - <i>Zoezi la 4.8.4:</i> Mada ya 4 ya Kitabu cha Wakufunzi. |
|------|--|---|--|--|
| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
| 3 | <p>Aina tofauti za viazi vitamu na sifa zake.</p> <p>Kuchagua, kuhifadhi na kuzalisha maradufu vipando vya viazi vitamu.</p> | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuwa na uwezo wa kutambua, kuchagua na kuhifadhi vipando salama vya viazi vitamu. - Kujua kanuni bora na mbaya za uchaguzi na utunzaji wa vipando vya viazi vitamu. - Kuelewa tofauti kuu zilizopo kati ya aina mbalimbali za viazi vitamu. - Kujua sifa za aina tatu za viazi vitamu zinazofaa kwa eneo, mkoa au kanda yao. - Kuwa na uwezo wa kuwasaidia wakulima kutambua na kutaja tabia za msingi wanazotafuta katika aina mbalimbali za viazi vitamu. | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 5.10.1: Miche ya kupandikiza: Salama na iliyozalishwa.</i> Zoezi la shambani la kutambua na kutaja vipando salama; chukua vipandikizi, jifunze namna ya kupandikiza katika kitaru cha kuzalishia, jadili namna ya kutunza, kukokotoa viwango vya uzalishaji wa miche (angalia Zoezi la 5.10.1.[saa 1 na dakika 5] - <i>Zoezi la 3.5.1: Tambua tofauti.</i> Zoezi la shamba ili kutambua sifa za aina mbalimbali za viazi vitamu hasa katika mashamba yaliyojirani nawe; kujadili na mkulima juu ya ni kwa nini analima aina mbalimbali za viazi vitamu; halafu anatomia viazi aina nyingi tofauti kufanya jaribio la kutathmini ladha (angalia 3.5.1). [saa 2 na dakika 45] | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 5.10.1:</i> Shamba lililojirani lililopandwa viazi vitamu ikiwemo miche au mashina yaliyocharibiwa na virusi na wadudu. Kitaru kilichopandwa nusu. Visu 5 vya kukatia; vifaa 2 vya kumwagilia vyenye maji ndani yake. Majembe mawili ya mkono. - Kitalu cha karibu cha uzalishaji wa haraka ambacho kimepandwa wiki 8 kabla ya mafunzo aina mbili ya viazi vitamu yenye viwango tofauti vya uzaaji. Chati mgeuzo na kalamu za wino mnene. - <i>Zoezi la 3.5.1:</i> Shamba lililo jirani likiwa na aina mbalimbali za viazi vitamu vilivyopandwa na ambalo washiriki watawuna baadhi ya viazi. Mahitaji mengine ni karatasi za A4, penseli, |

| | | | | |
|--|--|--|--|---|
| | | <ul style="list-style-type: none"> - Kufahamu ya kuwa upendeleo wa aina mbalimbali za viazi vitamu unatofautiana baina ya watu. - Kujulishwa juu ya ni kwa nini uangalifu unahitajika wakati wa kuvuna na umuhimu wa kilimo cha viazi vitamu. - Kupata uzoefu wa kufanya jaribio la ladha (kwa kutumia kadi za rangi nyekundu, njano, na kijani). | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 3.5.2: Kuchagua aina ya viazi vitamu.</i> Fanya mjadala katika makundi juu ya vigezo na sababu za msingi za kutofautisha aina mbalimbali za viazi vitamu, na zipi ni muhimu na kwa sababu gani? Washiriki watengeneze matangazo au zana za kufundishia aina kuu za viazi vitamu zinazoimwa katika eneo husika na pia zinafaa katika eneo fulani lengwa (angalia 3.5.2). [dakika. 70]. - <i>Wasilisho la 3.</i> Anuwai asilia ya viazi vitamu; kuelezea sifa za aina mbalimbali za viazi vitamu. [dakika 20] - <i>Wasilisho la 5a na 5b:</i> Kuchagua vipando, utunzaji na uzalishaji. [dakika 20] - <i>Zoezi la 5.10.2:</i> Mfumo wa S Tatu. Kufanya mazoezi ya mbinu ya S Tatu, kutoka hatua ya uchaguzi wa viazi hadi upakiaji na uwekaji katika sehemu kavu na yenye baridi. [saa 1 na nusu] | <p>vifutio, madaftari kwa ajili ya washiriki, nakala za kutosha za kitini cha maelezo kuhusu viazi vitamu (Kiambatanisho cha 3.1) na kukadiria kiwango cha vyanzo vya vitamini A kutoka katika aina ya viazi vitamu lishe rangi ya chungwa (Kiambatanisho cha 3.2), nakala za kutosha za fomu kwa ajili ya utunzaji shirikishi wa tathmini ya ladha ya viazi vitamu (Fomu nambari 5B na 5B 2 na Kiambatanisho cha 3.5b), majiko ya kupikia na mafuta ya kuwashia moto, sufuria, maji, viberiti, visu.</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 3.5.2:</i> Chati mgeuzo (angalau ukurasa mmoja kwa kila mshiriki), penseli za rangi ya kijani, kahawia, chungwa na njano kwa wingi; katalogi ya CIP kuhusu viazi vitamu rangi ya chungwa. |
| | | | <p>Zana na maandalizi ya awali kwa siku ya 3 vinaendelea:</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Wasilisho la 3</i> juu ya anuwai ya viazi vitamu, na sifa za aina mbalimbali za viazi vitamu. - <i>Wasilisho la 5a na 5b:</i> Kuchagua vipando, utunzaji na uzalishaji. - <i>Zoezi la 5.10.2:</i> Kuhusu viazi vitamu 200 — baadhi vikiwa vibovu na vya ukubwa mbalimbali. - Mabeseni 6 ya plastiki, magazeti, ndoo tano; fagio tano. Andaa Mfumo wa S Tatu miezi mitatu kabla ya kuanza kozi ya mafunzo kwa wakufunzi ili wanafunzi waone | |

| | | | <p>uchipuaji wa viazi.</p> <p><i>Maandalizi ya awali</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kwa Zoezi la 3.5.1: Bainisha shamba la karibu lililopandwa aina mbalimbali za viazi vitamu na baadhi ya mimea iliyoathiriwa na wadudu na magonjwa, kisha waone wakulima ili kufahamu kama wanakubaliana na suala la kutembelewa na washiriki mashambani mwao, na wenyewe kuhojiwa na washiriki na baadhi yao (kujaribu kupunguza idadi ya) miche kukatwa na kung'oa baadhi ya mimea kuona sifa za viazi na baadhi kuvionja, shina 1 hadi mawili kwa kila aina. Wakulima watapaswa kufidiwa kwa kila mmea unaovunwa au kung'olewa. <p><i>Kwa Zoezi la 5.10.2:</i> Fanya mipango na mwenye shamba ili washiriki watembelee, kuchagua na kupata vipando. Ni lazima liwe shamba lenye matatizo ya wadudu na magonjwa, ili washiriki wafanye uchaguzi hasi (kung'oa mimea yenye magonjwa na kutupa mimea dhaifu na kuchagua mimea yenye afya tu, na isiyo na wadudu wala magonjwa). Kuandaa kitaru cha uzalishaji haraka kilichopandwa vipando aina mbili wiki 8 kabla ya mafunzo na ambavyo viwango vyake vya kuzaa vinavyotofautiana mfano mita 1 ya mraba (miche 50) ya Aina A; mita 1 ya mraba (miche 50) Aina B. Andaa kitaru cha uzalishaji haraka shambani, ili washiriki waweze kumalizia na kufanya mazoezi ya kupanda vipando walivyopata, kuwekea kivuli na kumwagilia.</p> <p>Kwa Zoezi la 5.10.2: Andaa Mfumo wa 'S' Tatu miezi michache kabla ya kuanza Mafunzo kwa Wakufunzi, ili wanafunzi wagundue viazi na kuviona vikichipua, na wanaweza kuvitumia kufanya mazoezi ya kuvipanda.</p> | |
|------|--|--|--|---|
| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/ Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
| 4 | Usimamizi na uzalishaji wa zao la viazi vitamu. Magonjwa na wadudu waharibifu wa | <p><i>Washiriki waweze:</i></p> <ul style="list-style-type: none"> - Kuelewa hatua mbalimbali tofauti za mzunguko wa uzalishaji na ukuaji wa zao la viazi vitamu na maana yake katika usimamiaji wa kila hatua. - Kuweza kutafuta mifano halisi ya | <p><i>Zoezi la 7.9.1: Ukusanyaji wa viazi vilivyoathiriwa na wadudu waharibifu na magonjwa mashambani na kujifunza namna ya kudhibiti:</i> Ukusanyaji wa viazi vilivyoharibiwa na majani au matawi yenye ugonjwa, uchunguzi wa wadudu waharibifu</p> | <p>- Zoezi la 7.9.1: Shamba lililo jirani lenye mimea michanga ya viazi vitamu iliyoathiriwa na virusi na magonjwa ya viazi vitamu ambalo mwanzo lilikuwa limepandwa viazi vitamu, na viazi vitamu vilivyokomaa au vya umri mkubwa ambavyo washiriki wanaweza</p> |

| | | | | |
|-------------|-------------------------------------|--|--|---|
| | viazi vitamu na namna ya kudhibiti. | <p>wadudu waharibifu na magonjwa ya viazi vitamu shambani. Pia kuelezea na kuonyesha uharibifu unaosababishwa na kila mdudu na ugonjwa.</p> <ul style="list-style-type: none"> - Kufahamu kwa upana mbinu halisi za kivitendo za kudhibiti wadudu waharifu na magonjwa yanayoathiri zao la viazi vitamu. - Kuwasaidia wakulima wafanye jaribio kule shambani la kufananisha na kulinganisha aina nyingi tofauti za viazi vitamu na mbinu mbalimbali za kusimamia viazi vitamu. | <p>katika shamba la viazi vitamu, mjadala wa vikundi na kuchangiana mawazo kutafuta ni wapi wanakotokea wadudu na magonjwa na namna yanavyosambaa kwa kasi (ukihusisha nzi weupe kama inawezekana). Husisha mazoezi kwa vitendo na kujadili namna ya kuponya na kuondoa miche na matawi ya viazi vitamu yaliyoathirika. (Angalia 7.9.1). [dakika 75 pamoja na kusafiri]</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 6.9.1:</i> Kulinganisha aina mbalimbali za viazi vitamu na taratibu za usimamiaji: Kuandaa shamba darasa la viazi vitamu (angalia maelezo ya kina katika 6.9.1). [saa 3] - <i>Wasilisho la 6:</i> Mzunguko wa maisha ya wadudu, na magonjwa makuu ya zao la viazi vitamu (ikiwemo hatua za mavuno); washiriki wachore kwenye daftari zao mzunguko wa zao, na baada ya mjadala wajumuishe maelezo yanayopaswa kuzingatiwa katika kila hatua. [dakika 30]. - <i>Wasilisho la 7a na 7b:</i> Mzunguko wa maisha na udhibiti wa wadudu na magonjwa ya viazi vitamu. [dakika 45] | <p>kuvichunguza na kubaini mimea ya viazi vitamu iliyoathiriwa na wadudu na magonjwa. Yote haya yanaweza kufanyika kwa kutumia fimbo 20 za kuchimbia; ndoo 8 za kubebea na kusafirishia viazi vilivyoharibika; magunia 8; vyungu au majagi 20 yenye mifuniko yenye tundu kwa ajili ya kupitisha hewa; lensi mkuzo 20; washiriki lazima wabebe madaftari yao kwa ajili ya kuchukua kumbukumbu; penseli; chati mgeuzo na stendi yake; kalamu za wino mnene na gundi ya utepe.</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 6.9.1:</i> Chati mgeuzo, kalamu, kamba, tepu ya kupimia, koleo ya kuzolea, vikaratasi vya kutambulisha, vijifimbo na shamba lililo jirani la kufanyia majaribio, Mada ya 3, 6 na 7 ya Kitabu cha Wakufunzi kurasa za 20–22 katika kitini cha maelezo, ‘Ni nini kinachoniharibia viazi vitamu?’ - <i>Wasilisho la 6</i> juu ya hatua za makuzi ya viazi vitamu na shughuli za usimamizi. - <i>Wasilisho la 7a na 7b:</i> mzunguko wa maisha na udhibiti wa wadudu na magonjwa ya viazi vitamu. |
| Siku | Mada | Matarajio ya somo yaliyokusudiwa | Kazi/Shughuli za kufanya | Vifaa na maandalizi ya awali/tangulizi |
| 5 | Uvunaji, hifadhi, | <i>Washiriki waweze:</i> | - <i>Zoezi la 8.9.1: Kuongeza faida kwa</i> | <i>Zoezi la 8.9.1: Shamba la karibu la viazi</i> |

| | | | |
|---|---|---|---|
| <p>usindikaji na utafutaji masoko ya viazi vitamu lishe rangi ya chungwa.</p> <p>Kufanya mipango ya kuwafundisha wengine kuhusu 'Vyote Unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu'</p> | <ul style="list-style-type: none"> - Kujua mambo makuu yanayohusu uvunaji , usindikaji, na usimamizi baada ya mavuno. - Kuelewa ni vipi usindikaji na uhifadhi wa viazi vitamu rangi ya chungwa unaweza kuathiri viwango vya vyanzo vya karotini. - Kuelewa dhana ya masoko na mwelekeo wa soko. - Kuelewa fursa na changamoto za utafutaji soko la viazi vitamu lishe na bidhaa zake zilizosindikwa. - Kuanza kufikiria na kufanya mazoezi ya kuwasilisha kozi ya mafunzo ya siku 5 ya 'Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu'. | <p><i>kuhifadhi viazi vitamu vibichi.</i> Kazi ya shamba ya kuvuna viazi, kuvitenga vile vibovu; kutengeneza ghala la shimo la kuhifadhia viazi vitamu vibichi (<i>Angalizo:</i> Majani, nguzo za mianzi na miti kwa kufunikia inabidi iandaliwe mapema na shimo kuchimbwa kabla) (angalia 8.9.1). [saa 2]</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 8.9.2: Athari za kuanika viazi juani kwenye vyanzo vya karotini vya viazi vitamu lishe rangi ya chungwa.</i> Washiriki waangalie tofauti baina ya sampuli tatu za chipsi za viazi vitamu lishe rangi ya chungwa ambazo zimekaushwa kwa kutumia jua kwa muda wa siku 7, 5, au 2. Makadirio ya viwango vya vyanzo vya karotini vimetolewa ili kuonyesha jinsi vinavyopungua kadri muda unavyopita wakati wa uhifadhi (angalia 8.9.2). [dakika 30] - <i>Wasilisho la 8.</i> Uvunaji kidogokidogo, ukaushaji wa viazi vitamu vilivyokatwa vipande vidogovidogo kwa ajili ya kurefusha maisha na kukaa bila kuharibika; usimamizi wa baada ya mavuno ya viazi vitamu na chipsi zilizokaushwa; vyombo vya kuhifadhia, kinga dhidi ya wadudu na usimamizi wa muda mrefu. Jadili nani katika kaya anahusika na uhifadhi, na nini kinafanyika kuhakikisha kuwa taarifa inawafikia. [dakika 45] | <p>vitamu lililotayari kuvunwa na ambalo washiriki wanaweza kuchimba mashina hadi 10 kwa kila kikundi ili kukadiria mavuno; mizani; magunia; kikokotoo; kalamu na karatasi; chepeo, majembe; majani makavu; nguzo za mianzi, fimbo za kuvunia; matawi; nyasi za kuelekea na kamba.</p> <p><i>Zoezi la 8.9.2:</i> Viazi vitamu lishe rangi ya chungwa 50, mashine ya kumenyea, kichanja cha kuanika, chipsi za viazi angalau mikoba mitatu iliyosheheni sampuli, alama za kutambulisha, kalamu za wino mnene, seti ya taarifa inayoonyesha namna vyanzo vya karotini vivyopungua kutokana na kukaushwa juani kwa muda mrefu, nakala za kutosha za seti ya taarifa inayoonyesha namna vyanzo vyanzo vya karotini vinavyoweza kupungua kutokana na kuhifadhi kwa muda mrefu (Kitini cha 8.9.2a).</p> <ul style="list-style-type: none"> - Wasilisho la 8 juu ya uvunaji, ukaushaji, uhifadhi na masuala ya jinsia baada ya mavuno. - Wasilisho la 10a na b juu ya dhana ya masoko. - <i>Zoezi la 1.4.1:</i> Kadi zenye mada kuu za mafunzo ya wakufunzi ya siku 5 zilizoandikwa vyema. Washiriki wanapaswa kuwa na Kitabu cha |
|---|---|---|---|

| | | | | |
|--|--|--|---|---|
| | | | <ul style="list-style-type: none"> - <i>Majadiliano ya Kundi:</i> Usindikaji na mjadala kuhusu nani alengwe kwenye mafunzo ya usindikaji, watu kama wasindikaji wadogo na wanaoweza kutumia viazi vitamu lishe rangi ya chungwa kwenye shughuli zao. Mijadala kuhusu umuhimu wa kuhusisha wanaume japokuwa wanawake ndio watayarishaji wa chakula, lakini wanaume bado wana ushawishi mkubwa kuhusu ni chakula gani kipandwe au kinunuliwe. [dakika 10] - <i>Wasilisho la 10a na 10b:</i> Dhana ya masoko, mafunzo ya mfanyabiashara na mazingatio ya jinsia. [dakika 20] - <i>Zoezi la 1.4.1: Kufanya mazoezi ya kuwa mwezesaji wa mafunzo ya kujifunza kwa vitendo.</i> Fanya zoezi la kuwezesha mada kuu ya viazi vitamu, na kazi za vikundi juu ya kanuni za kutoa na kupokea mrejesho wenye tija (angalia Zoezi la 1.4.1.) [masaa 2 na dakika 30] - <i>Zoezi la 1.4.3: Kutathmini mafunzo.</i> Tathmini ya mafunzo (angalia Zoezi la 1.4.3) (Ni hiyari kurudia jaribio la ufahamu wa viazi vitamu kama jaribio la kuondokea (Kiambatanisho cha 1.2) [Saa 1]. - Utoaji wa vyeti. | <p>Wakufunzi cha ‘<i>Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu</i>’; madaftari na kalamu, vibandiko, chati mgeuzo, gundi ya utepe, kalamu za wino mnene pamoja na vifaa vingine vyote vilivyotumika katika programu ya mafunzo pamoja na viazi vitamu 100 vikiwemo viazi vitamu lishe rangi ya chungwa.</p> <ul style="list-style-type: none"> - <i>Zoezi la 1.4.3:</i> Nakala za kutosha za fomu za tathmini ya mafunzo namba 12.2.5c kwa kila mshiriki, kalamu, nakala za kutosha za jaribio la ufahamu wa viazi vitamu (Kiambatanisho cha 1.2) kama umepanga kufanya jaribio la kuondokea. - Vyeti vilivyokamilika, vinywaji baridi. <i>Maandalizi ya awali:</i> <ul style="list-style-type: none"> • Kwa Zoezi la 8.9.2: Siku 3 kabla ya kuanza rasmi mafunzo kwa wakufunzi; andaa kiasi kidogo cha chipsi za viazi vitamu lishe kisha vianike kwenye kichanja zikaushwe na jua (hii itakuwa sampuli ya ukaushaji wa siku 7). Siku moja kabla ya kuanza mafunzo kwa wakufunzi, ongeza vipande zaidi vya chipsi za viazi lishe, weka sehemu ileile uliyoweka vya kwanza lakini usichanganye na vile vya sampuli ya mwanzo. Hakikisha kuwa sampuli zimewekewa alama na ulinde zisiharibiwe. Siku ya tatu kati ya siku |
|--|--|--|---|---|

| | | | | |
|--|--|--|--|--|
| | | | | tano za mafunzo kwa wakufunzi, ongeza tena baadhi ya chipsi za viazi lishe halafu weka juu kwenye kichanja kilekile. Tumia hizo sampuli zote Siku ya 5 ya mafunzo kwa wakufunzi. |
|--|--|--|--|--|

13.3: Mawasilisho yaambatanayo na kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi ya 'Vyote Unavyopaswa Kujua Kuhusu Viazi Vitamu

Seti kamili za mawasilisho ya pawapointi zimeandaliwa pamoja na kitabu hiki. Inatarajiwa kuwa mawasilisho haya yatatumiwa kama ilivyopendekezwa katika siku ya 10 na 5 ya programu ya Mafunzo kwa Wakufunzi kama yalivyoonyeshwa katika vipengele vya 13.1 na 13.2.

Kozi hii ya Mafunzo kwa Wakufunzi imesanifiwa, hivi kwamba, kujifunza ni kwa vitendo zaidi, hivyo wawezeshaji wawe makini ili kuongeza mazoezi ya kujifunza kwa vitendo na kutumia mawasilisho tu kama kisaidizi. Ili kufupisha mada, kuonyesha picha za aina fulani ya wadudu na magonjwa au hatua zao na shughuli kama hazionekani shambani wakati wa mafunzo, na kusaidia kundi kujikita zaidi katika masuala muhimu kwa ajili ya mijadala zaidi.

Kuna wasilisho la kutumia pawapointi kwa kila mada katika kitabu hiki, na kwa baadhi ya mada ndefu kama vile Mifumo ya Mbegu, wasilisho limegawanywa kwenye vipengele kadhaa. Wawezeshaji wanaweza kuboresha mawasilisho haya ili kuyafanya yashabihiane zaidi na mazingira yao husika.

Kielelezo cha 13.1: Mfano unaoendana na slaidi za wasilisho la pawapointi kwa Mada ya 3 ya Kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi ya Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu

Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu

Wasilisho la 3. Aina mbalimbali za viazi vitamu na sifa zake

Kuwafikia Wakala wa Mabadiliko June 2013

Aina za viazi vitamu lishe zilizotoka karibuni

| Nchi | Aina ya viazi lishe zilizotoka karibuni |
|------------|---|
| Mozambique | Tio Joe, Namanga, Bela, Lourdes, Ininda, Irene, Cecilia, Erica, Delvia, Melinda, Amelia, Sumaia, Esther, Jane, Gloria |
| Tanzania | Mataya and Kiegea |
| Uganda | NASPO 8, Vita and Kabode |
| Rwanda | RW11—266 and RW11-2910 |
| Malawi | Zonden |
| Ghana | Bokye and Apomuden |
| Nigeria | King J and Mother's delight |

Ni vipi wazalishaji huzalisha aina mpya ya viazi vitamu?

Kungwa kwa ua (kupusha uchavuzaji/kiti mtuara)

Crossing block

Screenhouse

Mbegu ya kibotania au halisi ya mmea wa viazi vitamu

Amshamba darasa

Uchavuzaji kwa mkono

Utunzaji wa mbegu maabara

Jinsia na masuala anuwai kuhusu uchi aina ya viazi vitamu

- Wanawake na wanaume mara nyingi huvutiwa na sifa tofauti za viazi vitamu
 - Kwa mfao wanawak huvutiwa na sifa za mapishi wa viazi kama vile ufyonzaji kidogo na mafuta wakati wa kukaanga na hali ya kumeguka ya viazi vitamu. Wakati hujihusisha na mabao ya viazi, huvutiwa zaidi kuliko ilivyo kwa wanawake na sifa zihazohsiana na mambo ya masoko.
- Tathmini ya mahitaji ya viazi vitamu itasaidia kufahamu majukumu mbalimbali ya viazi vitamu katika masiha ya makundi mbalimbali katika jamii (mf. wanaume na wanawake, watoto, watu wa kipato tofauti, umri, na makundi ya dini).
- Mashamba darasa yanaweza kuandaliwa ikihusisha anuwai na uwakilishi wa makundi mbalimbali katika jamii
 - Uwakilishi wa kijinsia uwe na uwiano kwa wale wanaozalisha viazi vitamu katika jamii, hii pia itahusu makundi ya ufajiri wa kipato.
 - Pake ambapo wanawake ndio wazalishaji wakubwa wa viazi vitamu, shirikiana nao kutnedaji kazi. Hata hivyo waume zao wanapashwa kuilikwa katika vilao vya ufanyaji mipango ili kupata baraka zao kuelewa shaka zinazoweza kujitokeza
- Mikutano na shughuli za shamba vipangiliwe maeneo na muda ambao utakuwa muafaka na salama kwa wote watakaohusika wakiwemo wanawake

13.4: Kadi za kusaidia kumbukumbu za Kozi ya Mafunzo kwa Wakufunzi ya Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu

Zaidi ya hapo, seti ya kadi za kusaidia kumbukumbu zimeandaliwa kama zana za kusaidia ili kuambatana na kitabu na kozi ya mafunzo ya 'Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu'.

Kuna seti ya kadi ambazo zinazungumzia mada mbalimbali za mtiririko wa viazi vitamu. Kila kadi ina picha au mchoro upande wa mbele na maelezo muhimu yanayohusu mada upande wa nyuma. Inatarajiwa kuwa wawezeshaji watatumia seti hii ya kadi kama kijitabu muhimu/au zana ya kuwasilishia katika sehemu fulani wakati wa shughuli za mafunzo. Picha inaweza kuonyeshwa kwa wakulima/wakufunzi wakati mkufunzi akitumia maelezo upande wa nyuma ya kadi yaliyoandaliwa kama kisaidia kumbukumbu na wasibadilishe mazoezi ya mafunzo kwa vitendo kwa mijadala ya wakulima.

Kielelezo cha 13.2: Mfano wa upande wa mbele na wa nyuma wa kadi ya kusaidia kumbukumbu nambari 5.3



Mbele ya kadi ya kusaidia kumbukumbu nambari 5.3

Uhifadhi wa vipando vya viazi msimu wa kiangazi (Mfumo wa 'S' Tatu)

- Mfumo wa 'S' Tatu ni njia ya kuhifadhi vipando vya viazi vitamu msimu wa kiangazi.
- Uchuguzi wa viazi vidogo/ukubwa wa kati ambavyo havijaharibiwa na vilivyovunwa kutoka mashina yenye afya.
- Weka viazi kwa uangalifu kwenye beseni na kisha tengeneza matabaka yanayopishana ya mchanga baridi na viazi ukimalizia na mchanga juu yake.
- Weka chombo chako sehemu kavu, yenye ubaridi na salama mbali na kuku na watoto.
- Wiki 6 hadi 8 kabla ya mvua kunyesha, funua viazi vyako vilivyoanza kuchipua na kisha vipandikize kwenye kitaru cha bustani kuiancha nafasi ya 50*50 na kina cha 5 cm kwenda chini.
- Mwangilia kila siku 3-4 na baada ya wiki chache mizizi 40 inaweza kuzalisha vipandikizi 1,500 kuwahi mwanzo wa msimu wa mvua.

Mijumo ya mbegu za viazi vitamu 5.3

Nyuma ya kadi ya kusaidia kumbukumbu nambari 5.3

MADA YA 14: TAFAKARI

JUU YA

YYOYE UNAVYOPASWA KUJUA KUHUSU VIAZI VITAMU

Kutafakari ni sehemu muhimu sana ya mchakato wa kujifunza. Tunatarajia kuwa baada ya kozi hii na kitabu kufanyiwa majaribio, washiriki watatafakari kuhusu yale waliyoyafanya na kisha kubadilishana mawazo ya ni vipi kozi na kitabu vinaweza kuboreshwa. Ni muhimu zaidi kufikiria kwa makini uzoefu uliopatikana ili kuoanisha na mazingira husika. Unaweza kutunza mchakato wa tafakari yako kwa kila mada hadi siku ambayo itakuwa muafaka kwa tafakari hiyo kuwa na tija zaidi.

Kuna fomu mbili ambazo washiriki wanaweza kutumia kuratibu tafakari zao. Karatasi ya muhtasari wa jumla (Jedwali la 14.1) ambayo washiriki wanaweza kuijaza kila siku kuhusu tafakari za uzoefu walioupata kwenye kozi yenyewe au taarifa za awali kwenye kitabu cha mafunzo zinaweza kuboreshwa. Iwapo mshiriki angependa kutumia ukurasa mzima kwa ajili ya tafakari kwenye kila mada, Jedwali la 14.2 linatoa mwongozo ambao unaweza kutolewa nakala kwa ajili hiyo. Ni muhimu kuingiza nambari ya mada na kichwa cha habari juu ya kila ukurasa. Fomu hizi zinapatikana kwa njia ya mtandao kutumia Poto ya Ufahamu wa Viazi Vitamu [http://sweetpotatoknowledge.org/projects-initiatives/reaching-agents-of-change-rac/rac-tot-course-forms/Table%2014.1%20and%2014.2 Reflections%20on%20RAC%20ToT%20course.docx/view](http://sweetpotatoknowledge.org/projects-initiatives/reaching-agents-of-change-rac/rac-tot-course-forms/Table%2014.1%20and%2014.2%20Reflections%20on%20RAC%20ToT%20course.docx/view) .

Ikumbukwe kuwa kuna fomu za tathmini ya kozi (fomu ya 12.5.5c) ambayo imejumuishwa kwenye Mada ya 12 ya kitabu, ambayo pia inapatikana kwenye Poto ya Ufahamu wa Viazi Vitamu.

Baadhi ya makundi ya mafunzo yangependa kuunda kamati ndogo ya kutoa mrejesho ambayo ingekusanya maoni ya washiriki na kisha kuyafanyia muhtasari na kuyaingiza kwenye Jedwali la 14.1 au la 14.2, badala ya kila mshiriki kujaza fomu.

Makundi mengine yangependa kutumia maigizo kutoa muhtasari kila asubuhi kuhusu kile walichojifunza siku iliyopita, na maeneo ambayo bado yanawachanganya.

Vinginevyo, mwezeshaji anaweza kuwauliza washiriki kufikiria mambo matatu waliyojifunza siku ya leo na mambo matatu ambayo hawakuyaelewa kabisa siku ya leo, na kisha kuzungukia kila mshiriki kwenye chumba cha mafunzo na kumtaka ataje moja kati ya hayo. Mchakato huu unaweza kufanikiwa sana mahali ambapo kuna ushirikiano mzuri baina ya washiriki na mwezeshaji, na ambapo mwezeshaji ameonyesha kuwa muwazi katika maoni ya uboreshaji.

Tunatanguliza shukrani zetu kwa kutuletea maoni yoyote unayoweza kuwa nayo ya namna ya kuboresha mafunzo na kitabu kwa kutumia barua pepe kwenda kwa Jan Low (njia za mawasiliano zimeonyeshwa hapa chini). Tutayajumuisha kila inapowezekana.

Kwa: J.LOW@CGIAR.ORG

Kichwa cha habari; Tafakari juu ya Kitabu na Kozi ya Mafunzo ya Wakufunzi juu ya Vyote
Unavyopaswa Kujua Kuhusu Viazi Vitamu

Jedwali la 14.1: Karatasi ya muhtasari wa Jumla juu ya tafakari ya kozi ya mafunzo na Kitabu

| Tafakari ya Mafunzo ya Wakufunzi ya Vyote Unavyopaswa Kujua Kuhusu Viazi Vitamu | | | | | |
|--|--|--|---|---|-------------------------|
| Jina: | | Jinsia: | | Nchi na Mwaka: | |
| Nini kilikufurahisha zaidi kuhusu Mada hii? | Nini kiboreshwe na ni kwa njia zipi katika mafunzo haya | Nini kinakosekana katika mafunzo? | Nini kiboreshwe na ni kwa njia zipi katika kitabu? | Nini kinakosekana katika kitabu? | Maoni mengineyo? |
| Mada ya 1. Kuwasaidia watu wazima kujifunza | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 2: Asili na umuhimu wa viazi vitamu | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 3: Uchaguaji wa aina mbalimbali za viazi vitamu na sifa zake | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 4: Viazi vitamu vibichi rangi ya chungwa/njano na lishe | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 5: Mifumo ya mbegu za viazi vitamu | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 6: Uzalishaji na uangalizi wa viazi vitamu | | | | | |
| | | | | | |

| Nini kilikufurahisha zaidi kuhusu Mada hii? | Nini kiboreshwe na ni kwa njia zipi katika mafunzo haya | Nini kinakosekana katika mafunzo? | Nini kiboreshwe na ni kwa njia zipi katika kitabu? | Nini kinakosekana katika kitabu? | Maoni mengineyo? |
|--|---|-----------------------------------|--|----------------------------------|------------------|
| Mada ya 7: Udhibiti wa wadudu waharibifu na magonjwa yanayoathiri viazi vitamu | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 8: Usimamizi wakati wa mavuno na baada ya mavuno | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 9: Usindikaji na utumiaji | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 10: Masoko na ujasiriamali | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 11: Jinsia na mambo anuwai | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 12: Ufuatiliaji wa usambazaji na upokeaji wa viazi vitamu vibichi rangi ya chungwa | | | | | |
| | | | | | |
| Mada ya 13: Kutumia kitabu cha kozi ya mafunzo kwa wakufunzi ya Vyote Unavyopaswa Kujua Kuhusu Viazi Vitamu | | | | | |
| | | | | | |

Jedwali la 14.2: Tafakari kwa kila mada juu ya kozi ya mafunzo na kitabu kuhusu 'Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu'

| Tafakari kwa kila mada juu ya kozi ya mafunzo na kitabu kuhusu 'Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu' | | |
|--|---------|----------------|
| Jina: | Jinsia: | Nchi na mwaka: |
| Kichwa cha habari cha mada na nambari: | | |
| Nini kimekufurahisha zaidi kuhusu Mada hii? | | |
| Nini kiboreshwe na ni kwa njia zipi katika mafunzo haya | | |
| Katika Mada hii nini kinakosekana katika mafunzo? | | |
| Katika Mada hii nini kiboreshwe na ni kwa njia zipi katika kitabu? | | |
| Katika Mada hii nini kinakosekana katika kitabu? | | |
| Maoni mengineyo? | | |

VIAMBATANISHO
KATIKA
VYOTE UNAVYOPASWA KUJUA KUHUSU VIAZI
VITAMU

Yaliyomo

| | |
|---|------------|
| Viambatanisho..... | 399 |
| KIAMBATANISHO NAMBA 1. VIONGEZA NGUVU NA MZUNGUKO WA MAZOEZI KATIKA MAKUNDI NA MPANGO WA SHUGHULI YA MAFUNZO..... | 399 |
| <i>Kiambatanisho namba 1.1a. Viongeza nguvu</i> | <i>399</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 1.1b. Mzunguko wa mazoezi katika makundi.....</i> | <i>399</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 1.2. Jaribio la msingi la kutathmini hali ya ufahamu wa kilimo cha viazi vitamu.....</i> | <i>402</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 1.3. Mpango wa shughuli ya mafunzo</i> | <i>403</i> |
| KIAMBATANISHO NAMBA 2. JINSI YA KUTUMIA RASILIMALI YA MTANDAO WA PORTAL YA VIAZI VITAMU | 404 |
| KIAMBATANISHO NAMBA 3. VIFAFANUZI ELEKEZI KWA AJILI YA VIAZI VITAMU..... | 405 |
| <i>Kiambatanisho namba 3.1. Vifafanuzi elekezi kwa ajili ya viazi vitamu</i> | <i>405</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 3.2. Chati ya rangi ya viazi vitamu vyenye beta karotini</i> | <i>410</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 3.3. Karatasi iliyoandaliwa kwa ajili ya kukusanyia vielelezo vya kubainisha maumbile ya aina mbalimbali za viazi vitamu.....</i> | <i>412</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 3.4. Sampuli ya fomu ya mkataba wa makubaliano na mkulima kwa ajili ya majaribio shambani</i> | <i>412</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 3.5a. Fomu kwa ajili ya tathmini ya kabla ya mavuno na wakati wa mavuno hasa kwenye mashamba ya majaribio kwa njia ya utafiti.....</i> | <i>413</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 3.5b. Fomu kwa ajili ya ushiriki wa mkulima kutathmini ladha ya viazi vilivyotunzwa / hifadhiwa</i> | <i>420</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 3.5c. Fomu kwa ajili ya tathmini shirikishi juu ya ubora wa majani yaliochanua</i> | <i>422</i> |
| KIAMBATANISHO NAMBA 5. UTUNZAJI WA VIPANDO NA UTENGENEZAJI WA SHIMO/KIRARUKILILOFUNIKWA KWA WAVU..... | 424 |

| | |
|---|------------|
| <i>Kiambatanisho cha 5.1. Jinsi ya kusafirisha, kupokea, kuhimiliza, kupandikiza na kusimamia vipand vya tishu.</i> | <i>424</i> |
| <i>Kiambatanisho cha 5.2. Njia ya kitaru cha wavu halisi kinachofunikwa na chandarua kwa ajili ya kutunza vipando safi vya kuanzia.....</i> | <i>426</i> |
| KIAMBATANISHO NAMBA 6. KUTAMBUA AINA YA MCHANGA WAKO | 428 |
| KIAMBATANISHO NAMBA 11. VIGezo VYA KUONGOZA MCHAKATOWA HALI YA KIJINSIA | 429 |
| <i>Kiambatanisho namba 11a. Vigezo vya kuongoza mchakatowa kijinsia kwa ajili ya mahojiano katika makundi.</i> | <i>429</i> |
| <i>Kiambatanisho namba 11b. Vigezo vya kuangalia kwa ajili ya makundi ya wanawake na wanaume watawala/wasimamizi wa mashamba (Pale ambapo wanaume na wanawake wana mashamba tofauti ya viazi vitamu).....</i> | <i>432</i> |
| KIAMBATANISHO NAMBA 12. KARATASI YA MSINGI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA KILIMO CHA VIAZI VITAMU..... | 438 |

Viambatanisho katika Vyote unavyopaswa kujua kuhusu viazi vitamu

Kiambatanisho namba 1.Viongeza nguvu na mzunguko wa mazoezi katika makundi na mpango wa shughuli ya mafunzo

Kiambatanisho namba 1.1a. Viongeza nguvu

Viongeza nguvu hasani mazoezi mafupi ya kivitendo ya kuwatia nguvu na hamasa washiriki wote waliochoka katika makundi yao. Ifuatayo ni mifano halisi. Washiriki wanaweza kujua mifano mizuri zaidi ambayo wanaweza kutoa kwaushirikiano na wenzao katika makundi lengwa.

Kigezo ongofu kama taswira ya kujifunza kitu fulani

Washiriki wajichague wenyewe wakae katika makundi ya watu wawili wawilina katika kila kundi la watu wawili, waamue ninani kati yao atasimama kama kioo cha mwingine kujifunza kutoka kwake. Baada ya muda fulani, badilishaneni, mwingine awe kioo cha mwenzake naye ajifunze kutoka kwake.

Je, kuna mabadiliko gani?

Washiriki wanagawanyika katika makundi ya watu wawili wawili.Kila mmoja wa watu hawa wawili amchunguze mwenziwe na ajaribu kuvuta kumbukumbu ya muonekano wa mwenziwe kati yao. Halafu mmoja anageuka nyuma wakati mwenziwe anabadilisha muonekano wake; kwa mfano, kubadili saa na kuvaa mkono mwingine au kupandisha juu ya mkono wake, kutoa miwani yake usoni na kuzungushia nguo zake. Mwingine anajigeuza zaidi ya mara moja kuonyesha mazingira tofauti. Wote wawili watafanya hivyo kwa kupokezana.

Kiambatanisho namba 1.1b. Mzunguko wa mazoezi katika makundi

Ili kusaidia makundi ya watu kuwasiliana na kushirikiana kufanya kazi pamoja kama timu fanisi na halisia, michezo au mashindano yanaweza kutumika katika kuboresha mzunguko na mabadiliko bora ya makundi na kubainisha mambo muhimu ya msingi.

Kuongoza na kuwa mweledi wa wenye ulemavu wa kuona

Malengo mahsusi:Kupata uzoefu wa washiriki juu ya namna wanavyoguswa na mtu akiwa na ulemavu wa kuona, au kutokuwa na ufahamu wa baadhi ya mambo ya msingi yanayoendelea. Kujenga utayari na ufahamu kuhusu fikra na mahitaji ya msingi ya watu hasa wale ambao wanahitaji msaada. Kuimarisha uelewa wa watu kuhusu mahitaji ya msingi yatakayomfanya mshiriki kuwa mwezeshaji mzuri.

Vifaa vinavyohitajika: Vitambaa kwa ajili ya kufunika macho, vitambaa vyeusi hupendelewa sana kwani havipitishi mwanga.

Muda wa mafunzo: Dakika 15

Hatua kuu za kufuata;

- a) Waambie washiriki wakae katika vikundi vya watu wawili wawili, na baada ya hapo kila mmoja ajaribu kumfunga macho mwenziwe ili mtu asiweze kuona chochote.

b) Mtu ambaye yeye si mlemavu wa kuona amuongoze asiyeona wazunguke kwa muda wa dakika 5 (unaweza kuchagua njia yenye vikwazo na uwatake hawa walioongozana wabadilishane nafasi zao kulia/ kushoto kwa dakika 3).

Mjadala: Je, watu wenye ulemavu wakuona walijisikiaje pale ambapo hawakuwa wanaweza kuona? Je, ulifikiri nini na ulimchukuliaje mtu aliyekuwa anakuongoza katika mizunguko yote? Je, ulimwamini? Na kama ulimwamini, kwanini? Kama hukumwamini, ni kwanini? Je, unadhani mweledi kiongozi wako alikujali vilivyo au alikupuuza? Na kwanini unadhani alikujali? Na kama alikupuuza unadhani ni kwa sababu gani?

